

NABII MIKAYA

...?...mwaweza kuketi. Na—nawaambia, kama ningeishia kitu kama hicho, ningekuwa mtu mzuri. Ninataka tu kusema ya kwamba yeye ananipenda sana, hivyo ndivyo ilivyo, ananiwazia tu mema sana. Kamwe nisingeweza kuishia sifa kama hizo. Lakini nina furaha sana kujua ya kwamba mtu fulani anakuwazia mema namna hiyo.

² Wakati mmoja mimi, katika kanisa langu la nyumbani, nilikuwa nikihubiri kwa nguvu tu nilivyoweza na kujaribu kumfanyia Bwana jambo fulani, ndipo—ndipo nikatoka nje, mtu fulani akasema, “Niliufurahia ujumbe huo usiku wa leo, Ndugu Branham.”

Nikasema, “Asante. Asante, sana.”

Mtu fulani, mama, akakaribia, kasema, “Aisee, huo ulikuwa ni ujumbe mzuri sana, Ndugu Branham.”

Nikasema, “Asante. Asante.”

³ Kisha mtu mwingine akasema jambo fulani. Ndipo nikashuka, kulikuwako na mhudumu aliyetutembelea hapo, akasema, “Vema,” akasema, “Sipendi watu wanijivunie.”

⁴ Nikasema, “Vema, kuna tofauti moja tu,” nikasema, “Mimi hupenda.” Naye akasema...Nami nikasema, “Daima mimi hupenda kama mtu fulani akiniambia kama ninafanya mema ama mabaya, napenda kujua mahali ninaposimama.”

Akasema, “Vema, nisingetaka mtu yeyote aniambie kwamba nimefanya mema.”

Nikasema, “Mimi napenda,” kisha nikasema, “Ninaamini kuna tofauti moja tu kati yangu na wewe.”

Akasema, “Ni gani hiyo?”

Nikasema, “Ninasema ukweli, wewe husemi ukweli.”

⁵ Sote—sote tunapenda mtu atuambie kama tumeninii... Nami nafikiri mtu yeyote mzuri mwenye busara angefurahia ukosoaji mzuri, safi kama kweli umekosea, mtu fulani akwambie tu ume—umekosea na kukuonyesha mahali ulipokosea, ninathamini hilo. Ninataka kuwa sahihi, iwapo mtu anaweza kunifanya niwe sahihi.

⁶ Loo, kuna mambo mengi sana, nami ninataka kusema, hiyo ni, asante sana kwa ajili ya hizo pongezi, ndugu, na kadhalika. Na kila kitu ni sawa tu. Nakupenda vivyo hivyo, Ndugu Joseph. Nami ninatambua ya kwamba Ndugu Joseph amezuru taifa baada ya taifa, mahali baada ya mahali, akizishughulikia shule, na kuwatuma wahudumu, loo, shughuli chungu nzima za

maisha. Hakika nina heshima na upendeleo mkubwa mno kwa Ndugu Joseph Boze. Yeye ni ndugu yangu, kweli.

⁷ Basi, asanteni kwa kusema, “Siku njema ya kuzaliwa,” kwa maskini mke wangu mpendwa usiku wa leo. Alifika amechelewa sana asingengezwa kufika mkutanoni, lakini nitampelekea makaribisho hayo yote mazuri na kumwambia habari zake nitakapofika nyumbani, kule. Jinsi. . . Atafurahia hayo. Yeye yuko katika. . . Na hilo ni jambo moja, Ndugu Joseph alijivunia kidogo kunihusu, lakini yeye hakumjivunia kupita kiasi, maana yeye—yeye kweli anastahili kila kitu kingeweza kusemwa. Ana umri wa miaka arobaini na miwili leo. Yeye ni mtoto tu, mnaona, nilioa mtoto.

⁸ Na kwa hiyo, a—amesimama na mimi, hata hivyo, kama kipenzi halisi, halisi sana. Naye Billy, wakati mama yake alipokufa, nami nilikuwa na umri wa kama miaka ishirini na mitano, ishirini na sita, naye hakuwa na mama, akilia, huku sina mtu wa kumpelekea, naye alikuwa ni msichana mdogo tu, wakati huo, kama, yapata miaka kumi na saba, kumi na minane, alimtunza.

⁹ Na baadaye katika miaka, pasipo hata kuwazia zaidi juu ya kumwoa huyo mtoto si zaidi ya vile ningewazia mtu nisiyemfahamu akiketi huko nje, si kiasi *hicho*. Mimi na baba yake tulikuwa tukiwinda pamoja, nasi tulilelewa tu. Mbona, yeye, ningeninii, labda angenikemea, nami ningempiga kofi kwa ajili ya kipande cha peremende, basi hivyo ndivyo ilivyokuwa, mwajua, tulipokuwa, tukikua tu, watoto. Kwa hiyo tulikulua tu pamoja namna hiyo, wala kamwe sikuwazia kuhusu kumwoa.

¹⁰ Lakini nawaambieni, hakika ilikuwa ni zawadi niliyotumiwa na Mungu wakati mimi, wakati Mungu aliponipa mke wangu. Basi asanteni sana. Na kupitia hapo Yeye amenipa watoto watatu wa kupendeza.

¹¹ Naye alimchukua Billy Paul. Na kwa kawaida mama, mama wa kambo, kuingia, mnajua jinsi ilivyo kuhusu hilo. Ninaweza kusema hivi (Hayuko hapa, bali ni kweli, mtu yeyote anajua, ni, majirani zangu wako hapa.), kwamba anampenda mvulana huyo na amekuwa tu, alikuwa mwema kwake kuliko mama ya—yake. Nilimwona mama yake akimchapa makalioni wakati hakuwa na umri wa miezi sita, lakini Meda hajawahi kumgusa hata kidogo, ninii tu, alipaswa kuwa amefanya zaidi kidogo labda, ama, labda angekuwa tofauti. Aliniachia yote.

¹² Lakini, mimi. . . Watu wengine husema hawaamini katika kuwachapa makalioni, lakini mnajua Maandiko yanasema utaninii, usipotumia fimbo utamharibu mwanao, kwa hiyo ni—ni—ninaamini katika kuwarudi watoto, kuwafanya wajichunge. Tungalikuwa na zaidi ya hayo, tusingelikuwa na uhalifu mwingi sana wa vijana.

¹³ Sasa, usiku wa leo ni usiku wa Jumatano, nasi tunaninii, kwa namna fulani ni maskini usiku wakati sikuwa nikitarajia watu wengi sana kuingia, kwa sababu ya makanisa. Na usiku wa leo ni usiku wa mkutano wa maombi makanisani, nami, ninashukuru sana kwa—kwa ajili ya kusanyiko. Na ni jambo zuri kwamba wote wasije usiku ule ule, maana tusingeweza kufanya lolote nao. Nilisema muda mfupi uliopita, “Ni wangapi waliopo hapa, wakasema, ambao hawakuwahi kuwa mikutanoni hapo kabla?” Na ni zaidi ya nusu ya kusanyiko. Jana usiku kulikuwa na theluthi mbili yao ambao hawajawahi kuwa mkutanoni hapo kabla, na inaendelea.

¹⁴ Sasa, kuna mambo mengi sana ambayo tungeweza kusema. Ninaamini jana usiku, kama sijakosea, katika ujumbe wangu jana usiku nikizungumzia juu—juu ya, nasahau ni somo gani nililohubiri jana usiku, *kitu fulani* nilichokuwa nikiingiza kuhusu, loo, *Heri Iliyosahaulika*. Ninaamini hiyo ni Mathayo Mtakatifu, mlango wa 11 na ki—kifungu cha 6, ama kitu kama hicho, 11:6, naam, *Heri Iliyosahaulika*, “Naye heri awaye yote asiye chukizwa Nami.”

¹⁵ Nilikuwa nikihubiri juu ya jinsi watu wanavyochukizwa na Yesu. Naye Yohana alikuwa amekuwa, hakulielezea namna hiyo, lakini kwa namna fulani alichukizwa kwa sababu mambo hayakwenda jinsi alivyodhani yanapaswa kwenda, kwa sababu alikuwa amemtambulisha Yesu akiwa na, ama, Kristo, Masihi, akiwa na pepeto mkononi Mwake, na kuisafisha sakafu, na kuyachoma makapi, ndipo wakati alipokuja, Yeye alikuwa mpole sana na mnyenyekevu, na mnyofu. Na kwa hiyo wao. . . ilikuwa vigumu kwake kuelewa ni nini, kwamba hiyo ilikuwa ni nini. Inaonekana kana kwamba alikuwa ameabishwa, naye alikuwa, kwa namna fulani kidogo ni chukizo.

¹⁶ Hata hivyo alikuwa ameiona ishara ya Masihi na kujua ya kwamba ilikuwa ni Yeye, kwa hiyo akawatuma wanafunzi waone kama Huyu alikuwa Ndiye. Sasa, hilo lilikuwa baya sana kusema jambo kama hilo, lakini Yohana alikuwa ametiwa mafuta kwa roho ya Eliya, naye Eliya karibu ashikwe na fadhaa, pia, mwajua, chini ya mretemu. Naye huyu hapa Yohana, maadamu umesimama hapo ukilitoa, ni sawa, lakini inapokubidi kulingiza ndani, basi ni tofauti kidogo, unaona, kwa hiyo, Yohana gerezeni, jicho lake la tai lilikuwa limeingia utando.

¹⁷ Na kwa hiyo tuliona ya kwamba Yesu kamwe hakumpa hotuba yoyote, ama kumwambia jinsi ya kuninii, kumwambia Yohana, kulifanya, Yeye alisema tu, “Kaeni mkutanoni mpaka utakapokwisha mwone kitakachotukia.” Ndipo baada ya mkutano kwisha, Yeye alisema, “Sasa, nendeni mkamwonyeshe Yohana mambo haya: Viwete wanatembea, vipofu wanaona, viziwi wanasikia, kadhalika, na maskini wanahubiriwa injili. Na heri yeye asiye chukizwa Nami.” Kisha, akaanza kuzungumza juu ya chukizo.

¹⁸ Halafu basi nilikuwa, nilimtaja mtoto mdogo aliyekuwa ametoka Zion, Illinois, hapa juu. Na kama sijakosea, mtu fulani aliniambia, ama alisema walidhani walikuwa, ya kwamba huyo mtoto alikuwa humu jengoni usiku wa leo. Hiyo ni kweli? Hivi huyo mama yuko hapa pamoja na mtoto huyo aliyetoka kwenye Jiji la Zion, Illinois, aliyekuwa na mguu uliolemaa, uliopinda chini yake, na sasa anatembea? Alikuwa ama awe hapa usiku wa leo au kesho.

¹⁹ Huyo ndiye mama yake. Mungu akubariki, Dada. Ulikuwa hapa jana usiku? [Dada huyo anasema, “Ndiyo, nilikuwa.”—Mh.] Vema. Ni sawa. Sikuninii—sikuninii—mimi, ulielewa ninalomaanisha, kwamba hukuwa ukileta chukizo, bali ulikuwa tu, ulishangaa tu ni kitu gani kitakachompata mtoto huyo. Hiyo ni kweli? Vema. Bwana alifanya yale tu aliyosema angefanya, sivyo? Hilo ni zuri sana. Mshukuru Bwana kwa ajili ya jambo hilo. Unaye huyo mtoto mchanga? [“La.”] Hayuko hapa.

²⁰ Vema huyo, maskini mama huyo alitoka nje. Imani yake ilijengeka kabisa, loo, jamani, mara tu nilipomwekea mikono mtoto huyo mchanga, ilikuwa inaenda kutendeka papo hapo. Lakini mnaona, hiyo kweli, wakati mwingine, kama sisi, kama hiyo ni imani ya kweli, hakuna kitu kitakachoizuia. Kwa hiyo huko nje kwenye trela, maskini huyo mama akamleta mtoto huyo mchanga kesho yake, naye kwa namna fulani alikuwa akishangaa, yeye na maskini mumewe, na alitaka kujua ni kwa nini mguu wa mtoto huyo haukushuka.

Vema, kamwe sikusema chochote, nami nikawazia, “Yeye anaamini hilo, naye huyo msichana kweli anaamini hilo, kwa hiyo ha—halina budi kutukia, mradi tu . . .”

Alipotoka nje, aliniambia jambo fulani, “Unafikiri, Ndugu Branham, ni mapenzi ya Mungu kwa mtoto wangu kuwa mlemavu?”

Nami nikasema, “La, bwana, sivyo.” Hilo ndilo tu alilokuwa akingojea. Mnaona? Kwa hiyo Yeye akaiheshimu na kumponya huyo mtoto mchanga.

²¹ Na nikija tu dakika chache zilizopita, huenda nikakosea katika ushuhuda huu, lakini kuna, kama mwanamke huyo yuko hapa, nilifikiri niliona hilo gari huko nje, na trela, kulikuwa na mama aliyekuja kanisani mwangu hivi majuzi, yapata, loo, haijawa zaidi ya mwaka mmoja ama miwili iliyopita. Naye mama huyo alikuwa huko nje, namna *hii*, akiwa na uvimbe. Loo, hamjawahi kuona uvimbe kama huo! Madaktari hata wasingeweza kuugusa, ilikuwa ni hali mbaya sana, na mbaya sana hata asingeweza kutembea, iliwabidi kumbeba.

²² Vema, alisikia nitakuwa kanisani usiku huo. Nanyi mnajua jinsi ilivyo, ile maskani ndogo pale, kwa hiyo baada ya ibada kwisha sikuwaombea wagonjwa, niliomba tu, na—na nadhani alikuwa, kwa namna fulani alichukizwa pia. Lakini

hata hivyo, mmoja wa mashemasi waaminifu na baadhi yao, walijua nilipotoka kwenye chumba cha kusomea, ama, ofisi ya shemasi, huko nyuma. Walimbeba maskini mwanamke huyu pale, mwanamke mkubwa mno, na huo uvimbe mkubwa, loo, mbaya sana, nao wakamlaza chini pale kwenye vipandio, ambapo nitakapotoka ama ingenibidi kumkanyaga, au kitu fulani.

²³ Kwa hiyo basi nilipotoka, yeye alinena neno, ndipo Mungu akanipa Neno, nami nikalinena pia. Na yapata—yapata majira ya kiangazi yaliyopita, naamini ndivyo, alisimama mbele pamoja na mumewe, wakiwa njiani kurudi California, na mwanamke huyo ni laini kabisa, uvimbe huo ulikuwa umekwisha kabisa.

²⁴ Kuna . . . na kama hiyo . . . ni—nilimwona huko Bloomington hivi majuzi, nami nikasema, “Dada, ningetaka u—usimame usiku wa leo.” Ndipo baadhi ya wahudumu wakanishika, nami nikaanza kuzungumza, na kusahau jambo hilo. Nafikiri hilo ni gari lake la trela limewekwa hapa nje likiwa na leseni ya California. Kama mwanamke huyo yuko hapa ndani, waweza tu kuinua mkono wako, Dada? Popote, naam, huyo hapo huko nyuma. Hiyo ni kweli. Je, ungetaka kuingia kwenye marefu ya kanisa hapo kwa muda mfupi tu ili watu waweze kuona? Fungua koti lako, kusudi watu waweze kuona ninii yako . . . ? Akiwa na uvimbe mkubwa sana uliokuwa umetokeza nje sana. [Dada huyo anashangilia—Mh.] Kama—kama huyo angekuwa ni wewe katika hali hiyo ungeweza kujisikia hivyo pia.

²⁵ Sasa, kumbukeni, alikuwa mkubwa sana hata asingeweza kutembea huku na huku, namna *hii*, iliwabidi kumbeba, huku uvimbe umetokeza namna *hii*. Na kila chembe yake ilitoweka, ikaondoka, nayo imetoweka. Mnaona? Sasa, hatuninii . . .

²⁶ Kuna mama mwingine, nafikiri, humu jengoni usiku wa leo, nesi aliyesajiliwa. Nilimwona yeye na mumewe hivi majuzi hapa, hao ni marafiki wangu wa karibu.

²⁷ Kuona utachukua muda gani: Wakati kwenye kumbukumbu za Houston, Texas, yeye, matumaini ya mwisho, akifa, ameliwa na kansa, nao wakamleta mkutanoni. Ndipo wakati ndugu yangu, Howard, alipokuwa akisambaza kadi za maombi usiku huo, kwa kawaida yeye huja mbele, kama vile Billy angefanya, na kuzichanganya kadi, na kuwapa watu kadi za maombi. Naye mwanamke huyu, akiketi pale, alimwangualia mama mwingine mbaya kuliko alivyokuwa, nesi huyu, huku akiwahurumia wagonjwa, akaamka na kwenda mpaka nyuma kabisa na kujitafutia kiti huko nyuma kabisa.

²⁸ Usiku huo wakati Howard alipoingia, ndugu yangu, kusambaza kadi za maombi upande wa mbele, Roho Mtakatifu alisema, “Rudi, ukazisambaze huko nyuma, usiku wa leo.” Ndipo akapata kadi ya maombi, akaingia mstarini, Roho Mtakatifu akamwambia habari zake, kisha akamponya kabisa

kabisa. Naye, hiyo imekuwa yapata miaka kumi, kumi na miwili iliyopita, ama labda zaidi, naye angali ni nesi aliyesajiliwa, akisimamia hospitali ndogo ya binafsi huko Texas.

²⁹ Ndu-... Dada Harris, uko hapa usiku wa leo? Yeye ni nesi aliyesajiliwa, mahali fulani, mwanamke mzuri, mrembo kutoka... huyu *hapa*, hiyo ni kweli, nesi aliyesajiliwa. Hatua za mwisho za kansa, madaktari walioshughulikia ugonjwa huo kule chini wanajua walikuwa wamemkatia tamaa. Na sasa, wananiambia ya kwamba madaktari, wanaostaafu na kadhalika, humjia wapate usaidizi, wakijua ya kwamba yeye ni Mkristo mcha Mungu aliyeyatoa maisha yake kwa Kristo naye Mungu akamponya.

³⁰ Loo, ninajaribu kusema nini, rafiki? Usiudhike. Yeye, hana maudhi ndani Yake, Yeye anafanya kazi moja kwa moja kwa ratiba, um-hum, naam, bwana.

³¹ Ndipo Roho Mtakatifu alituongoza kusema jana usiku, ya kwamba hatuko huko nyuma kabisa, wala hatujasonga mbele, kabisa tuko kwenye wakati uliokusudiwa, Ujumbe huu wa wakati unaofaa tulio nao leo hii.

³² Na kama mtu fulani alisema, “Loo, hizo ni siku zilizopita,” na mtu kama huyo, nenda ukamwambie Yohana, mchungaji wako, ama yeyote yule, unaona, viwete wanatembea, vipofu wanaona, vivimbe vinatoweka, na kansa zinaponywa. Unadumu kwa muda gani? Kadiri tu unayouamini. Hiyo ni kweli. Huo ndio muda wokovu unaodumu, kwa hiyo, kadiri tu unavyouamini.

³³ Kwa hiyo sasa iweni na moyo wa ushujaa, mwaminini Mungu. Wala Kristo hajatuacha, msiudhike, kama Yeye aliliahidi, Yeye atalifanya, Naye yuko kwenye wakati uliokusudiwa hasa, kweli kabisa, Yeye yuko moja kwa moja kwenye wakati uliopangwa kila mara.

³⁴ Nawe unasema, “Ndugu Branham, ninahisi usiku wa leo ni usiku wangu ninaoenda kuponywa.” Usijali, Yeye yuko moja kwa moja kwenye wakati uliopangwa, wewe kaa tu kwenye wakati uliopangwa, na kama unaamini huu ndio usiku wako, huu ndio.

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu wa maombi.

³⁵ Baba wa Mbinguni mwenye rehema na Mtakatifu, tunapokikaribia kiti Chako cha rehema, tupe neema Yako usiku wa leo, kuhubiri Neno la Mungu, kusudi watu wapate kuona na kuamini, kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

³⁶ Nilipokuwa nikiomba... Watu waliomleta mke wa—wangu alasiri ya leo, na mvulana wangu mdogo, Joseph, wako hapa jengoni mahali fulani, nadhani waliingia. Alikuwa ni Shahidi wa Yehova, naye mke wake, nafikiri, alikuwa ni wa Anderson Church of God. Alikuwa na kifua kikuu, akaponywa,

alikuwa na mwana mlemavu, polio miguuni mwake, mguu wake ulipinda. Nao wakaufuatilia huo mkutano, walikuwa huko Houston, Texas, naamini. Huko ndiko Dada yetu Harris (Popote alipokuwa, kuna giza pembeni, popote alipokuwa, *kule.*) alipoponywa. Nao walikuwa huko usiku huo ambapo ile Nuru ilishuka.

³⁷ Walikuwa Louisville, waliishi nje ya, Kentucky, nao wakaingia. Naye Ndugu Wood mwenyewe, nadhani, hayazingatii sana, akiwa ni Shahidi wa Yehova, na aliyelelewa katika familia ya namna hiyo, na kuamrisha vikali asiyakaribie makanisa, na kadhalika.

³⁸ Lakini alimwona msichana usiku huo aliyekuwa amegeuzwa kuwa ninii, aliyekauka tu kama jiwe, na kwa muda wa miaka mingi alikuwa hawezi, ukaenea hata karibu na nyonga zake, wala asingeweza kutembea kwa miaka mingi. Akasimama kutoka hapo, akatembea jukwaani, akajitwika machela yake, akaenda zake nyumbani, akafanya kazi, akakimbia huku na huku kwenye vipandio kesho yake.

³⁹ Mvulana mdogo aliyeketi kwenye kiti cha magurudumu, mguu mmoja mrefu kuliko huo mwingine, alisimama, akaja jukwaani na kusimama pale, maskini huyo jamaa alihubiri moja kwa moja kutoka jukwaani, miguu yote miwili sawa. Basi hilo likawachangamsha.

⁴⁰ Kwa hiyo nikaenda Sweden, nikarudi, nao walikuwa hapa mahali fulani mkutanoni, mahali fulani hapa Ohio, nao walikuwa wameketi huko nyuma kabisa nyuma ya hema. Usiku huo Roho Mtakatifu akasema, “Mvulana mdogo kule nyuma aliyevaa sweta, sweta ndogo ya manjano, mama na baba yake,” na yote kuwahusu. Wao, hata kamwe, walijua kamwe sijawahi kusikia habari zao, hata kidogo, yeye alikuwa mkandarasi huko Kentucky. Kisha kasema, “BWANA ASEMA HIVI, huyo mvulana kiwete ameponywa.”

⁴¹ Vema, wakaketi pale kitambo kidogo na mara akamwambia mumewe, “Acha huyu mvulana asimame,” kitu kama hicho. Ndipo mvulana huyo akasimama, nayo miguu yote miwili ilikuwa sawa. Mvulana huyo ni kijana mwanamume usiku wa leo, ameo, ana mtoto. Na kama sijakosea, David, uko humu jengoni? David Wood, uko wapi? Mguu mmoja umekunjamana chini yake na huo mwingine. . . Hivi uko hapa, David? Huyo hapo, amesimama mlangoni. Naomba ushuke tu uje upande huu kidogo, David, kusudi waweze kuona hakuna. . . Hata hajui ulikuwa ni mguu upi, nao ulikunjamana chini yake.

⁴² Sasa, yule dada kutoka Zion, pale, uliye na huyo mtoto mchanga, unaona kile Mungu alichofanyia mmoja wa hiyo miguu iliyokunjamana, unaona yale anayokufanyia, Yeye angali ni Mungu, Yeye yuko moja kwa moja kwenye wakati uliopangwa.

Jambo pekee tunalopaswa kufanya ni kuipanga tu imani yetu pamoja na uwepo Wake hapa, nalo litatukia.

⁴³ Sasa, kwa ajili ya ujumbe mfupi tu. Naye Billy alinipongeza jana usiku, kwamba kwa kweli nilimalizia yapata dakika thelathini na tano, arobaini. Nimekuwa nikichukua saa mbili, zaidi kidogo. Lakini a—alisema, “Unaendelea vizuri, kama ukiweza kupunguza ufikie dakika ishirini itakuwa bora kwa watu.”

⁴⁴ Nami nikasema, “Vema, hilo litakuwa gumu kwangu.” Na kwa hiyo, mnaona, kwa namna fulani ni vigumu. Ninayo mengi, ya kuzungumzia, maana nina Bwana mkubwa mno ajaye, nami ninalipenda sana ninaendelea tu kuzungumza.

⁴⁵ Lakini ninyi mnaotaka kuangalia katika Maandiko, kama mtaingia katika Wafalme wa Kwanza, mlango wa 22, kifungu cha 14, kifungu hicho kimoja kwa ajili ya fungu dogo la kufanya muktadha, kama Bwana akitusaidia kuzungumza, kwa dakika chache tu.

*Mikaya akasema, Kama BWANA aishivyo, neno lile
BWANA aniambialo, ndilo nitakalolinena.*

⁴⁶ Sasa, tuna hadithi kuu hapa mbele zetu, lakini hamna wakati wa kuliendea kwa njia ifaayo. Basi kesho usiku, nikiweza, Bwana akipenda, ama usiku mmoja, ni—ningetaka kurudi kwenye Agano la Kale, hapa, na kuchukua makala juu ya manabii na kuyatoa, Yeye akipenda. Ndipo mimi, inaonekana kama Yeye amekuwa akinishughulikia, nipate kuchukua Alhamisi na Ijumaa usiku na kuhubiri *Alama Ya Mnyama Na Muhuri Wa Mungu*, nalo ni jambo lifaalo kwa wakati huu nafikiri kanisa linapaswa kujua.

⁴⁷ Na sasa, katika jambo hili tunaona ya kwamba kulikuwa na mfalme katika Israeli wakati huu jina lake Ahabu. Alikuwa ni mfalme wa Israeli, na kwenye wakati uu huu Yehoshafati alikuwa mfalme wa Yuda. Naye Yehoshafati alikuwa ni mtu mwenye haki, mtu mcha Mungu, naye baba yake, Asa, aliyemtangulia, alikuwa ni mtu mcha Mungu.

⁴⁸ Lakini tunaona ya kwamba Ahabu alikuwa kwa namna fulani kile tunachokiita mwaminio mkwamia mpakani, jamaa mwenye haki ambaye kwa namna fulani alienda, njia yoyote upepo uliyovuma, mbona, ulimchukua Ahabu. Naye alikuwa na mke jina lake Yezebeli, naye alikuwa amemwoa msichana huyu ili tu kuimarisha ufalme wake. Naye alikuwa ni mwabudu sanamu, naye alikuwa ameivuruga Israeli kabisa.

⁴⁹ Na, vema, wahubiri wote walikuwa wameenda, wale waliokuwa wahubiri wazuri sana, walikuwa wamekuwa vuguvugu, na—na karibu wote walikuwa wamerudi nyuma. Lakini kulikuwa na mzee mmoja wasingeweza kumgeuza, huyo alikuwa ni Eliya, hakuwa akimdanganya, kwa hiyo a—alidumu

moja kwa moja pamoja na Neno hilo, na kwa hiyo, alikuwa ametabiri kuhusu yale ambayo yangempata Ahabu.

⁵⁰ Kwa hiyo basi siku moja Yehoshafati aliiitwa huko kumtembelea mfalme huyu wa Israeli, ambao, walikuwa tu ni kama ndugu, Wamethodisti, na Wabaptisti, na Wapresbiteri, Wapentekoste, walikuwa ni ndugu, wote walikuwa ni jamii ile ile na ni wale wale, ilivyodhaniwa, *wakimtumikia* Mungu yeye yule. Naye Ahabu alikuwa, angali alikuwa ni mwaminio, vuguvugu, mwaminio mkwamia mpakani. Lakini mke wake alikuwa, alikuwa ndiye kiongozi wa nyumba, bali hapana shaka alikuwa ndiye shingo iliyokidhibiti hicho kichwa, mwajua, kwa hiyo lolote alilosema, yeye alikuwa ndiye mfumo wenyewe.

⁵¹ Na, ndugu, hebu niseme hili kwa heshima kwa baadhi yenu Wanademokrasia wazuri wenye msimamo mraba: Hicho ndicho tulicho nacho sasa. Huenda yeye akawa sawa, bali kuna mfumo huko nyuma unaokidhibiti hicho kichwa. Nasi tulifanya jambo lile lile kama tu. . . Tatalifikia hilo baadaye.

⁵² Kwa hiyo, hata hivyo, mwanamke huyu, alimwongoza tu, chochote alichotaka, alimwendea tu na kumfanya afanye hivyo, alijifunga kwenye kidole chake, naye akaitawala nchi, alikuwa ndiye mamlaka nyuma ya hicho kiti cha enzi.

⁵³ Na kwa hiyo Yehoshafati alialikwa huko chini kumtembelea Ahabu, naye Ahabu akamwonyesha fahari yote ambayo Israeli walikuwa nayo. Sasa, hapo ndipo mwaminio anapoweza kuingia kwenye kundi baya. Wakati Yehoshafati aliposhuka kwenda kufanya ushirika na Ahabu aliingia upande mbaya.

⁵⁴ Sasa, kuna wakati mwingi sana ambapo watu wanaweza kufanya hivyo wakiwa na nia njema. Watu hawamaanishi kufanya mabaya. Ninaamini kuna watu wengi usiku wa leo walio katika dhambi ambao kweli hawataki kufanya hivyo.

⁵⁵ Wakati fulani uliopita msichana mdogo mrembo, katika chumba cha wendawazimu, nao walikuwa na chumba cha dharura, nami nikarudi kule, mwanamke mrembo sana kama niliyepata kumwona, nikaangalia kote kwa baadhi ya hao wendawazimu, naye akasema, “Waweza kunichukua kwanza, Ndugu Branham?”

Ndipo nikawazia, “Ati kukuchukua kwanza? Wewe si mmoja wa—wa wagonjwa,” na, bali alikuwa.

Naye akaniambia jinsi alivyokuwa ameishi, nikamwambia, nikasema, “Hutaki kufanya hivyo, sivyo?”

Akasema, “La, bwana, sitaki, kitu fulani hunisukuma kufanya hivyo.”

Nikasema, “Huenda likaonekana la mtindo wa kale, bali huyo ni ibilisi.”

⁵⁶ Naye akasema, “Daima nimeamini hilo.” Ndipo Mungu akamkomboa huyo mwanamke, ameolewa na ana watoto usiku

wa leo. Naye alikuwa ni mlevi, mlevi sugu, kahaba, loo, kamwe hujawahi, maisha ya kuchukiza namna hiyo. Lakini inaninii tu, hawataki kufanya hivyo lakini kitu fulani kinawasukuma kufanya hivyo, hawataki kufanya hivyo.

⁵⁷ Nilishuka nikaenda huko Bowery na kuwachukua walevi hao, na kusema, “Vema, jina lako ni nani?”

“Utaninunulia pombe?”

“La, sitakununulia pombe, mimi ni mhudumu.”

⁵⁸ Kisha kasema, “Hebu simama na uangalie *huku*, nawe unaweza kuona benki niliyokuwa rais wake.” Mnaona? Huo ni ukweli mwingi. Mnaona? Lakini wa—wao hawataki kufanya hivyo, kitu fulani huwasukuma kufanya hivyo.

⁵⁹ Nina rafiki anayeketi humu ndani mahali fulani, labda usiku wa leo, yeye sikuzote huja, na nyinyi, karibu nyote, mnamfahamu Rosella Griffith. Alikuwa mmoja wa walevi sugu wakubwa sana Chicago iliokuwa nao, makazi ya wasokwao hayakuwa na kitu kwa Rosella. Ndipo akaja kwenye mkutano wa Hammond, na huko Roho Mtakatifu akamwita na kumwambia yote kulihusu, naye akakombolewa kutoka kwenye huo ulevi sugu, na sasa anafanya kazi kwenye magereza na kadhalika pamoja na walevi sugu wengine.

⁶⁰ Rosella, uko wapi, Dada? Uko humu jengoni usiku wa leo? Naam, huyu hapa, papa *hapa*, na m—m—mtakatifu wa Mungu, mtu mzuri sana, aliyeyatoa maisha yake na kujisalimisha kwa Kristo, na sasa . . .

⁶¹ Nilipomwona akija jukwaani (Samahani, Dada Rosella.), alikuwa ni mchawi mwenye macho ya kipopo, mwenye sura mbaya sana, kumwona. Loo, hujawahi kumwona mtu mwenye *sura kama hiyo*. Nami ninawatakeni mninii. . . Sisemi hili ili kumpendeza, lakini Rosella, usiku wa leo, ni msichana mzuri, mrembo, anayependeza, ana miaka kumi na mitano, anaonekana mdogo kuliko alivyo hasa kwa miaka kumi na mitano, ishirini. Na—naye ni mtu wa kupendeza sana, na kamwe hakunywa pombe, wakati hospitali baada ya hospitali, na daktari baada ya daktari, Shirika la Walevi Sugu la Chicago, wote walimkatia tamaa kama mgonjwa asiye na matumaini, naye huyo hapo ameketi usiku wa leo, baada ya miaka na miaka.

Neema ya ajabu! jinsi inavyosikika tamu,
Inayomwokoza mwovu kama mimi!

Jambo ndilo hilo.

⁶² Enyi walevi, mnaona yale Mungu anayoweza kufanya? Wagonjwa wa kansa, mnaona yale Mungu anayoweza kufanya? Miguu mifupi, viwete, mnaona yale Mungu anayoweza kufanya? Yeye ni Mungu. Yeye hachelewi.

⁶³ Sasa, tunaona ya kwamba mtu huyu aliingia kwenye kundi baya.

64 Nawe mwenye dhambi, unawasikia watu hao wakipaza sauti, ulimwona mwanamke huyo akikimbia kule na kuanza kuja huku na ule—ule uvimbe mkubwa mno, amejaa utukufu sana asingeweza ku- . . . hata asingeweza kusema chochote ndipo akaanza kunena kwa lugha? Mbona, alikuwa amejazwa sana na nguvu za Mungu, zilizokuwa zimeutoa huo uvimbe ndani yake, huo, mbona, asingeweza kuzungumza lugha yake mwenyewe, alikuwa tu akimsifu Mungu. Mnaona?

65 Unashangaa ni kitu gani kinachowafanya wafanye hivyo. Vema, hebu upate tu kitu kile kile basi, kisha uangalie kile kitakachokufanyia. Unaona? Litakuwa ni jambo lile lile. Kwa hiyo Yeye yuko kwenye ratiba hasa, “Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili ya watoto wenu, na kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjje.”

Unasema, “Mchungaji wangu, kanisa langu, haliamini hilo.” Vema, wewe ni, uliingia katika kundi baya, uliingia katika kundi baya, unaona.

66 Hivyo ndivyo Yehoshafati alivyofanya, aliingia katika kundi baya. Alipata mapambo mengi sana, naye Ahabu akamwonyesha vitu vyote vinavyometameta vya . . .

Nadhani huenda Yehoshafati alisema, “Ati bado unamwamini Ye- . . . ?”

“Loo, mbona, bila shaka, tunamwamini Yehova, bila shaka, bila shaka.”

“Vema,” akasema, “sasa . . .”

67 Unapouona ulimwengu ukikualika mahali fulani, kumbuka, wana sababu ya kibinafsi. Unaona? Nawe msichana, wewe hapa unayetoka kwenye nyumba ya Kikristo, ambaye hujawahi kuvuta sigara wala kunywa pombe, naye msichana huyo anajaribu kukupa sigara, ana sababu yake ya kibinafsi. Kijana huyo anayetaka kukupeleka nje ukacheze dansi, ana sababu yake ya kibinafsi. Unaona? Angalia tu. Kaa mbali na kundi hilo. Kaa mbali nalo.

68 Haidhuru wanaonekana kuwa wema jinsi gani, “Jitengeni na ubaya wa kila namna,” Biblia ilisema. Kaeni mbali nao. Usiangalie jinsi—jinsi unavyoweza kuikaribia bila kutenda dhambi, angalia jinsi unavyoweza kukaa mbali nayo, hilo ndilo jambo la kufanya. Kamwe usiangalie jinsi unavyoweza kuikaribia dhambi, angalia jinsi unavyoweza kukaa mbali nayo.

69 Kama vile yule Mskoti alivyokuwa ambaye alikuwa anataka kwenda kuvuka mlima, walikuwa na madereva watatu kule, mmoja wao akasema, akasema, “Vema, ule ufa mkubwa!” Akasema, “Hiyo ndiyo barabara ya kwenda *kule* juu?”

Akasema, “Hiyo ndiyo barabara.”

Kasema, “Vema, hiyo barabara ina upana gani?”

Akasema, “Barabara ile ina upana wa inchi kumi tu kuliko magurudumu ya ndani, ya gari, sehemu zingine.”

Kasema, “Afadhali uchague dereva hodari.”

Akasema, “Sina budi kuupanda huu mlima, niupite.”

⁷⁰ Mtu mmoja akasema, “Ninaweza kuendesha farasi wangu kwa mwendo wa shoti, na pamoja na ninii, nichukue mjeledi wangu na kuwaendesha farasi wangu shoti, nami nikae ndani ya inchi mbili za ule ukingo kotekote, bila kuanguka.”

Huyo dereva mwingine akaja na kusema, “Ninaweza kukaa ndani ya inchi tatu kutoka kwenye ukingo huo, na kuuzunguka katika mwendo wa kasi sana.”

Jamaa huyo mwingine, huku amesimama tu pale, akichokoa vidole gumba vyake. Kasema, “Nawe je, bwana?”

Kasema, “Bwana, huenda nikaweza kufanya hivyo, bali sitaki kubahatisha namna hiyo, mimi hukaa tu mbali na huo upande kadiri utakavyo.”

⁷¹ Akasema, “Mimi ni abiria *wako*.” Hiyo ni kweli. Basi hivyo ndivyo ilivyo, usione kile unachoweza kufanya kupita nayo mbele za Mungu, angalia jinsi unavyoweza kukaa mbali na dhambi, na maumbo yote, na maagizo, na kutokuamini, na ujiepushe na kila kitu kisicho cha kiungu. Kiondokee, usikikaribie.

⁷² Nami nafikiri kama mtu amewahi kuwa katika Nchi ya Kanaani na kuonja mambo mazuri ya Mungu, haikubidi kuwa na wasiwasi sana juu ya huyo mwanamume ama mwanamke kuhusu jambo hilo, watakaa mbali nalo, mradi tu wamewahi kuonja hizo zabibu nzuri za Kanaani.

⁷³ Sasa, Yehoshafati alishuka naye Ahabu akamwonyesha mapambo yote ya huo ufalme, na sasa, alikuwa na sababu zake za kibinafsi, naye akasema, “Je, unajua ya kwamba Ramoth-gileadi ni mali yetu, huko juu? Wakati Yohua alipozigawa nchi, wewe ni shahidi wake, naam, bwana, kwamba wewe ni shahidi kwamba tulipewa *hiyo*, na mfalme wa Shamu ameimiliki, nayo ni mali yetu.” Kasema, “Sasa, hiyo si ni kweli?”

Akasema, “Hmm, hiyo ni kweli, hakika, kwamba sisi sote ni Waisraeli.”

Akasema, “Sasa, utaunganisha jeshi lako na jeshi langu? Basi sote wawili pamoja, tutakwea kule juu na kumfukuza atoke humo, maana hiyo ni yetu.”

⁷⁴ Basi, mnaona, wanaweza kuonyesha, ulimwengu unaweza, ibilisi anaweza kukuonyesha baadhi ya sababu nzuri sana zinazometameta, na hata kuliingiza katika Maandiko, um-hum.

“Naam,” aseme, “vema sasa, sisi sote ni wenye haki, sisi sote ni watoto wa Mungu. Watu wote ni wana wa Mungu.”

Loo, la! La, la, la.

“Sote tunaamini mambo yale yale.”

Loo, wala sivyo. La, bwana, hakika hatuamini yale yale.

⁷⁵ Na kwa hiyo, wao, mwajua, Yuda aliambiwa, kasema, aliamriwa kuishindania *ile* imani kwa bidii, si imani *fulani*, *ile* imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja. Hiyo ni kweli. Si kuishindania imani *fulani*, *ile* imani waliyokabidhiwa mara moja. Basi unapokuwa na imani hiyo, Yesu alisema ishara hizi zitafuatana na hao walio na imani hiyo. Basi *hiyo*, ndipo unajua mahali unaposimama, unaona, na ndipo unajua ungeishi maisha ya namna gani.

⁷⁶ Kwa hiyo Yehoshafati akasema, “Mbona, hakika, hata hivyo, sisi ni watu wale wale,” kasema, “magari yangu ni magari yako, na—na farasi wangu ni farasi wako, na—na askari wangu ni askari wako, mbona, hakika, sote tuko pamoja.” Kasema, “Kwa nini tusikwee tu kule juu,” [Ndugu Branham alikohoa—Mh.] (Samahani.) “nasi tutawafukuza?”

⁷⁷ Lakini kasema, kisha akageuka, hapana shaka aliwazia, “Vema, ngoja kidogo, hatujamwomba Bwana kuhusu jambo hili.” Mnaona, mwaminio halisi, kabla hajafanya lolote, haidhuru nini, jinsi linavyoonekana ni zuri, daima atamtaka Mungu shauri kwanza. Amina. Naam, bwana.

⁷⁸ Mwajua, nimeona, mara nyingi watu hunijia na kusema, “Loo, Ndugu Branham, kama utakuja huku, tutakuwa na udhamini mwingi sana, tutafanya *mengi sana*, tutahakikisha kamwe hakutakuwa na senti moja itakayosalia bila kulipwa, nasi tuta—tutakupa *kiasi fulani* kila usiku.” Inametameta sana, lakini mwajua, tumbili hurukia vitu vinavyometameta, kwa hiyo hebu tungoje tu. Dhahabu ya mjinga hung’aa kuliko dhahabu halisi.

⁷⁹ Mwajua, hivi majuzi usiku nilisema ya kwamba Kristo ni mwe—mweko, si mng’ao. Kamwe hatutaweza kuuongoa ulimwengu kwa kujaribu kuyang’arisha makanisa yetu, na kuyafanya makubwa zaidi, na kuwaadabisha wahudumu wetu kwa elimu bora, wa—wao tayari wana vitu hivyo vyote. Wana kila namna ya saikolojia na michezo ya mpira na kila kitu, ulimwengu una hayo. Lakini sisi tuna Kitu fulani wasicho nacho, hicho ni Kristo. Mnaona? Jaribu, kaa tu katika eneo lako mwenyewe. Tunaye Kristo, hawana Kristo, wana saikolojia yote. Au usijaribu kujilinganisha akili na wao, huwezi kufanya hivyo, wao—wao hawaninii, wanaweza kukushinda.

⁸⁰ Hebu mwendee kasisi wa Kikatoliki wakati mmoja, jaribu kumshinda akili. Yeye ana vitabu mia sita, vitakatifu tu kama Biblia hii, anavyopaswa kujifunza. Kwa hiyo, ndugu, kamwe usijaribu kujilinganisha akili naye, nitakwambia hilo. Lakini kama utadumu tu na Roho Mtakatifu, atafanya yaliyosalia, unaona, wewe dumu tu na Huyo. Unaona? Lakini hatupaswi

kujilinganisha akili, tunapaswa kuwa na Kristo, Huyu ndiye tuliye naye, tuna Kitu ambacho hawana.

⁸¹ Kwa hiyo unapaswa sikuzote kumtaka Bwana shauri kabla hujafanya lolote. Ndipo unaposema utafanya jambo fulani, huna budi kusema, “*Kama* ni mapenzi ya Bwana,” huna budi kusema, “ikiwa ni mapenzi ya Bwana.” Biblia inatwambia hivyo.

⁸² Yehoshafati alikumbuka mafundisho yake mazuri ambayo baba yake alimpa. Akasema, “Hivi hudhani inatupasa kumtaka Bwana shauri?”

⁸³ Ninaweza kumwazia Askofu Ahabu akisema, “Loo, loo, mbona, mbona, bila shaka, naam, bwana, na—na—naamini inatupasa kufanya hivyo. Vema sasa, ninalo hilo kundi moja kwa moja hapa chini, kwa sababu nina—nina kundi zima la wahubiri hapa chini, manabii.” Sasa, kumbukeni walikuwa ni manabii. “Nina shule nzima ya hao hapa chini.”

“Vema. Hao ni manabii wa aina gani?”

“Manabii wa Yehova; tunao papa hapa. Na, vema, nitaenda niwalete.”

“Vema, hilo litakuwa sawa.”

⁸⁴ Kwa hiyo wote wakaja, naye Hezekia na hao wote, nanii, yeye alikuwa ndiye kiongozi wa ninii, miongoni mwao, askofu mkuu. Kwa hiyo wakati wote walipokuja mbele ya hao wafalme, nao wameketi huku wamevaa majoho yao ya kifalme, mwajua, kufanya, huko nje katika namna fulani ya mahali palipotengwa karibu na lango, basi hao manabii wakaja, mia nne wao, hebu wazieni, wanafunzi mia nne, si wanafunzi, walikuwa maaskofu waliowekwa wakfu, jamaa wakubwa, wao wakasema, “Tumeomba, tumefunga, tunayo mapenzi ya Bwana, BWANA MUNGU YEHOVA ASEMA HIVI: ‘Kwea ukaitেকে,’ kwa kuwa ni mali yetu, na ni yetu, nasi tuna haki ya kuimiliki. Hima twendeni tukaiteke.”

Wanasema, “Hebu tuliwazie hilo sasa. Sasa, kiakili, hiyo ni kweli. Tulipewa hiyo sisi, um-hum, hiyo ni kweli.”

⁸⁵ Na sasa hao manabii, “Hebu tuone sasa, katika saikolojia yetu, mawazo yetu, nia yetu ya kiakili, hiyo ni mali yetu, Mungu alitupa sisi, ni mali yetu, taifa la kikafiri linaimiliki.”

“Unawaona manabii wangu? Kila mmoja wao anasema, ‘Kwea ukaitেকে.’”

⁸⁶ Na, mwajua, mtu ambaye amewahi kuwasiliana na Mungu mara moja, kwa—kwa namna fulani anaweza kujua kama ni la Mungu au la. Mwajua, Yehoshafati kidogo alijisikia, kigeni kidogo, akasema, “Uh, uh, uh, hivi huna mmoja zaidi?”

⁸⁷ Akasema, “Ati mmoja zaidi? Mbona, hao hapo mia nne walioelimika zaidi ya wote, waliofunzwa vizuri kuliko wote, waliovalia nadhifu kuliko wote, na, mbona, waliopo nchini,

ulimwenguni! Kama watu mia nne kwa sauti moja wanasema, ‘Nenda,’ mbona unauliza mmoja zaidi?”

Lakini kulikuwako na hisia ndogo ya kigeni mle ndani, mwajua, kulikuwa na kasoro fulani.

⁸⁸ Kwa hiyo jinsi gani, mnaona sasa, unapoanza kuwazia ya kwamba—ya kwamba kama sote tukikusanyika pamoja katika umoja, mbona, kuna nguvu, lakini huenda isiwe ni aina sahihi ya nguvu. Mnaona? Palipo na umoja pana nguvu, palipo na makubaliano. Hiyo ni kweli, kama limekubaliwa juu ya jambo sahihi, naam, tutaambatana na hilo, lakini hebu lirudi kwenye Neno la Mungu kwanza. Mnaona? Na kwa hiyo wakasema . . .

⁸⁹ Hivyo ndivyo madhehebu yetu ya kwanza yalivyopata kuundwa, kanisa letu maarufu la Katoliki. Hapo ndipo wanaposema, katika madhehebu, “Baraza la Nikea kule, hivi hudhani kule Nikea kwamba wanapaswa kujua, wakati hao wote, nao waliwashinda kura hao wengine na kuliingiza hili kwa kura?” Sivo, bado haikulifanya kuwa sahihi. La, bwana.

⁹⁰ Nalo ni sahihi wakati Mungu anaposema ni sahihi, na si sahihi mpaka Yeye aseme ni sahihi. Hiyo ni kweli kabisa. Haidhuru ni kubwa jinsi gani na limedumu muda gani.

⁹¹ Kasisi mmoja aliniambia si muda mrefu uliopita, kasema, “Mbona, Ndugu Branham,” ama, “Bw. Branham,” hakuniita “Ndugu Branham,” akasema, “Bw. Branham, inakuthibitishia kanisa Katoliki ni sahihi,” kasema, “angalia dhoruba ambazo limestahimili, kote katika nyakati, namna hiyo.” Watu wangu hapo awali walikuwa Wakatoliki, mwajua, kwa hiyo, nikiwa Mwairishi. Kwa hiyo wanasema, “Kotekote,” kasema, “angalia kile kanisa Katoliki limestahimili, mateso yote, kotekote.”

⁹² Nikasema, “Hilo si fumbo, taifa zima na kila kitu kikiwa nyuma yake. Lakini vipi kuhusu Pentekoste, huku likipingwa na kila kitu, lingali linaendelea?” Amina, hiyo ni kweli, likipingwa na kila kitu, hakika. Kila kitu kikiwa *upande* wa kanisa Katoliki, hakika, lingeweza kuendelea hivyo. Lakini vipi kuhusu kila kitu dhidi yake, na kuwanyonga, na kuwaua, na kadhalika? Lilidumuje? Nalo hili hapa leo, likiangaza kama dola, amina, kama nyota za mbinguni, na litadumu milele.

⁹³ Sasa, angalieni, huyu Yehoshafati, alisema, “Kuna kasoro kidogo,” chini moyoni mwake alihisi kuna kasoro fulani. Kasema, “Lakini hivi una nabii mwingine mmoja tu mahali fulani?”

Kasema, “Naam, nina mmoja. Ni Mikaya huko nje, yeye ni mwana wa Imla, lakini,” kasema, “Ninamchukia.”

Loo-loo! Alijua papo hapo alikuwa kwenye mkondo sahihi, akasema, “Loo, mfalme asiseme hivyo. Nenda kamlete.”

94 “Vema, tuna haja gani na mmoja zaidi, wakati dhehebu lote—wakati dhehebu lote linasema ni kweli?” Hilo bado halilifanyi kuwa sahihi, hata kidogo, hata kidogo, la.

Akasema, “La, bado sina budi kuninii, kumwona nabii huyu mwingine.” Kwa hiyo akasema, “ulisema jina lake ni nani?”

Kasema, “Mikaya, yeye ni mwana wa Imla.”

95 Kasema, “Vema, nendeni mkamlete, he—hebu tusikie atakalosema juu yake,” maana kulikuwako na hisia ndogo, ya ajabuajabu ambayo haikukubaliana na Neno, mahali fulani.

96 Kwa hiyo wakatuma mtu. Ahabu akamvika askari na kumtuma huko, naye akamkuta Imla huko nje mahali fulani, ama, si Imla, hasa, ninamaanisha Mikaya, mwana wa Imla, alikuwa huko nje mahali fulani mwituni katika kibanda kidogo mahali fulani, akasema, “Sasa, Mikaya. Je, wewe ndiye nabii Mikaya?”

Akasema, “Naam.”

Kasema, “Je, ulijua unaenda kuheshimiwa?”

“Loo, ninaenda kuheshimiwa?” Kana kwamba Mungu hakuwa tayari amezungumza naye, mwajua. Kwa hiyo akasema, “Ati ninaenda kuheshimiwa?”

97 “Ndiyo, naam, utalikwa kwenye shirika la—la makasisi litakalokusanyika pamoja, na wote wamekutanika huko chini kwa mfalme, nawe unaenda kwenye Ikulu. Nakwambia, Mikaya, kamwe usingewazia ungepata heshima kama hiyo, lakini kweli umeipata, maskini jamaa mdogo, asiye na elimu kama wewe unayeketi hapa nyuma, bali wanataka kukuleta kwa, mbele ya mfalme. Na wao—wao, ninii, sikiliza sasa, hivi unajua mahali ilipo ile shule kubwa ya manabii, lile shirika kuu la ulimwenguni kote la shirika la wahudumu?”

“Naam,” kasema, “Uh-huh, ninawajua wote, naam, najua habari zao, huko chini.”

“Vema, unajua, bila shaka unamjua Hezekia kule, yule nabii mkuu, kiongozi wa hao wote?”

“Naam, nimesikia habari zake, naam, mtu mashuhuri, wanasema.”

“Naam, ndivyo alivyo, nao wanasema ana L.L., Ph., D.D.D., Q.U.S., mambo haya yote, wajua.”

“Naam, najua unachomaanisha.”

98 “Vema, yeye pamoja, hao wote, kwa nia moja wamekuja na kuombea jambo fulani, wakafunga na kuomba, naye amejitengezea pembe mbili kubwa za chuma, ana hakika, ana Neno la Bwana.” Kwa hiyo akasema, “Alikuwa mbele za mfalme, akuchukua pembe hizi kubwa, na kusema, ‘Kwa hizi utawasukuma Washami moja kwa moja watoke kwenye ardhi ya Mungu, nasi tutamiliki mali ya Mungu. Amina.’”

⁹⁹ Hivyo ndivyo tulivyowazia katika madhehebu yetu, tulikuwa tunaenda kusukuma kila kitu nyuma na kuwafanya wote wa Umoja, tulikuwa tuwafanye wote wa Utatu, tulikuwa tunawafanye wote Assemblies of God, tulikuwa tuwafanye wote Baptisti, ama Methodisti, lakini pembe zetu za chuma hazifanyi kazi. Hiyo ni kweli, hiyo ni kweli. Hulifanyi hivyo, huwasukumi huku na huku, la, “Utawasukuma nyuma na kuiteka, umiliki kitu hicho.”

¹⁰⁰ Mfumo wetu wa kimadhehebu ni sawa mradi tu humkatilii mbali jamaa huyo mwingine, lakini unapomkatilia mbali huyo ndugu mwingine, umekosea. Kwa hiyo hivyo ndivyo walivyofanya, hivyo ndivyo madhehebu, msingi wake wenyewe ni, ni kumkatilia mbali jamaa huyo mwingine.

¹⁰¹ Kwa hiyo basi, tunaona, basi, ya kwamba yeye alisema, “Vema, kama shirika hilo lote la wahudumu linasema,” kasema, “sasa, nitawaambia, nina neno kutoka kwa yule nabii mkuu, alisema, wewe sema jambo lile lile alilosema. Ukifanya hivyo, ushuke uje huko, tutakuingiza kwenye hili shirika, tutakufanya tu mmoja wetu, naam, tuta—tutakwambia, tutakuunganisha moja kwa moja na makundi yetu, kama uta—utasema tu jambo lile lile analosema.”

¹⁰² Lakini, ndugu, alimwambia mtu tofauti, Mikaya akasema, “Nitasema tu yale Mungu asemayo, na hakuna lingine.” Amina, napenda hilo, naam, bwana: “Nitasema tu yale Mungu asemayo.”

Kwa hiyo hatimaye wakashuka kule wakafika mbele za mfalme.

Naye Mikaya alikuwa amekesha mbele za Bwana usiku uliotangulia, aone yale angesema.

¹⁰³ Basi wakaenda mbele za mfalme, nayo hii hapa shu—shule yote ya manabii imesimama, nao wote walikuwa wamesimama pale wakitabiri. Sasa, kumbukeni, wao hawakuwa manabii makafiri, walishuhudia kuwa ni manabii wa Yehova. Lakini hebu angalieni tu sasa.

Kwa hiyo wakaona ya kwamba baada ya wao kusema yote, wote walikuwa wametabiri, kasema, “Naam, Bwana angali anasema kwea, Yeye yu pamoja nawe, uteke huo mji.”

Mikaya akaangalia kote, akasema, “Endeleeni, mkauteke huo mji.”

Ahabu alijua kulikuwa na kasoro kidogo katika jambo hilo, akasema, “Ni mara ngapi inanibidi kukuapisha?”

Akasema, “Hakika, kwea, ukauuteke huo mji, lakini,” akasema, “niliwaona—niliwaona Israeli wametawanyika kama kondoo kilimani, bila mchungaji.” Mnaona?

¹⁰⁴ Ahabu, hilo lilichochea hasira yake ya haki, akasema, “Nilikwambiaje? Atatabiri maovu, yote anayozungumzia, akiwahukumu wanawake wetu kwa kuvaa kaptura,” naye

akiwa pale, “mambo haya yote anayotwambia juu ya ninii yetu yote... Nilijua daima atasema jambo baya kunihusu mimi, hakika kadiri anavyosimama pale, hivyo ndivyo atakavyosema.” Angeweza kusema nini nyingine?

Akasema, “Niliwaona kondoo wa Israeli wametawanyika kilimani, kama kondoo wasio na mchungaji.” Na—na loo, jamani, alijua ilimaanisha kifo chake.

Naye akasema, loo, alipandwa na hamaki, kwa sababu a—alisema, “Nilikwambia atatabiri mabaya.”

¹⁰⁵ Vema, angwezaje kufanya jambo lingine lolote? Kwa sababu alilijaribu ono lake kwa Neno la Mungu, naye alijua ya kwamba Neno la Mungu lilikuwa limemwambia—limemwambia Ahabu kupitia kwa Eliya, ambaye kweli alikuwa nabii wa Mungu, kwamba mbwa watairamba damu ya maskini Ahabu kondeni, ama, kwenye gari, kwamba mbwa watairamba damu ya Ahabu. Naye Mungu alikuwa dhidi ya Ahabu, basi mtu huyu wa Mungu angewezae kubariki kile Mungu alichokuwa amelaani?

¹⁰⁶ Jinsi yeye, mhudumu anawezaje kusimama mimbarani na kuwaambia watu, mambo wanayofanya, na kuwaacha waendele bila kusema lolote kulihusu? Ni zaidi ya ninavyoweza kusema.

¹⁰⁷ Mnajua, huko Uchina, mungu wao mkuu huko chini ni mwanafalsafa wa kale wanayemwita Confucius. Confucius ni *neni* katika Uchina. Marekani ni *confusion*, [Kiingereza: Confusion lina maana ya machafuko—Mfa.] badala ya *Confucius*.

¹⁰⁸ Loo, ilikuwa kwamba unachukua picha... Nilienda wakati mmoja uliopita mahali fulani kula, mtu fulani akaniuliza, na ilionekana kwangu kana kwamba mvulana wangu mdogo, Joseph, alikuwa ameingia kwenye ndoo ya rangi mahali fulani ya aina mbalimbali za rangi na kuchafua ukuta wote. Nikasema, “Mahali pazuri kama hapa huku pakiwa na kitu kinachoonekana kichafu, kinachoonekana chenye madoa mabaya namna hiyo kikining’inia ukutani?”

“Loo,” nikamwuliza huyo mhudumu wa kike, akasema, “vema huo, wewe, huo uko kwenye turubai.”

Nikasema, “Hakika unaonekana kama, umekuwa chini ya matone ya rangi yanayodondoka kwenye ngazi mahali fulani ambapo yangefanya namna fulani ya mapambo.”

¹⁰⁹ Akasema, “Loo,” akasema, “bwana, huo ni wa *Fulani-wa-fulani* na *Fulani-wa-fulani*.” Mbona, hata haukuonekana kama mchoro hata kidogo. Naye akasema, ninasahau ni ngapi, mamia ya dola ambazo mchoro huo uligharimu, kwenye ukuta huo.

¹¹⁰ “Vema,” nikasema, “Kama ingekuwa ni mimi, ningetoa kiasi kama hicho kuuondoa hapo,” nikasema, “kwa sababu ungenitia wasiwasi hata kufa, unaonekana wa kuchukiza sana.”

111 Mnajua, ilikuwa kwamba nyeusi ni nyeusi na nyeupe ni nyeupe, ukizichanganya pamoja unapata kijivu. Kwa hiyo hivyo ndivyo tu ilivyo, wamechanganyikana sana, uko wapi mpaka kati ya mema na mabaya? Wamethodisti wakiwa sahihi, vipi kuhusu Wabaptisti? Kama Presbiteri ni sahihi, vipi kuhusu Pentekoste? Kuna Mpaka mahali fulani, nao Mpaka huo ni Neno la Mungu, hilo ni Neno, Mpaka wa Mungu ni Neno Lake, “Neno la kila mtu na liwe uongo, na Langu, Kweli.”

112 Kwa hiyo tunawezaje kubariki kile ambacho Mungu amelaani? Mnawezaje kuwaruhusu wanaume kuoa mara mbili au tatu na ni mashemasi makanisani mwenu? Mnawezaje kuwaacha wanawake wakate nywele zao, na kuvaa kaptura, na kuvalia kizinifu kabisa, waje jukwaani, na kucheza piano, na kutoka nje mitaani na kutembea huku na huku namna hiyo, wala msiseme neno kulihusu? Huwezi kulikomesha, bali unaweza kutoa neno dhidi yake. Kweli. Na asilimia tisini na tano wao huvuta sigara, na kufanya yasiyofaa, na kunywa bia.

113 Nilikuwa katika chu—chuo fulani si muda mrefu uliopita, na kwenye maeneo ya chuo kikuu wasichana wakitembea huku na huku, wamevaa kaptura na makopo ya bia yametapakaa kila mahali, huku wahudumu wakicheka, wakiidhihaki Injili. Vema, unawezaje kutarajia kizazi kijacho. . . ? Watakuwaje? Uko wapi mpaka?

114 Nilikuwa na maskini rafiki wa Kimethodisti, Dk. Spurgeon, alizoea kuimba wimbo:

Tulilegeza kamba,
Tukapatana na dhambi.
Tulilegeza kamba, kondoo wakatoka nje,
Lakini mbuzi waliingiaje?

115 Wakati mlipolegeza kamba, hilo ndilo lililosababisha jambo hilo. Mkaondoka na wazo la ajabuajabu la kijana jeuri asiye na heshima huko chuoni aliyejua mengi kulihusu kuliko—kuliko Mungu Mwenyewe alivyojua, kisha mkaanzisha fundisho juu ya kitu kama hicho. Rudini kwenye Neno!

Haidhuru, mnasema, “Vema ni, li—li—linasema *hivi*, linafanya *hivi*.”

116 Halina budi kuwa ni Neno la Mungu kote kote, Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele, si mungu aliyekufa, Mungu aliye hai, si yule aliyewaponya wagonjwa huko nyuma, yule anayewaponya wagonjwa sasa. Ina faida gani kuzungumza juu ya Mungu wa kale, iwapo Yeye si Mungu yule yule leo? Bila shaka.

117 Sasa, huwezi kupata joto kwa moto wa kuchorwa, basi kitu fulani ambacho unasema, “*Ilikuwa* hivyo wakati mmoja.” Hatuna budi kuwa na kitu fulani *sasa*, na Mungu yuyo huyo angali anaishi, na angali anaponya, angali anaokoa, angali

anatoa Roho Mtakatifu, na Yeye, na ni Yesu Kristo yeye yule, jana, leo, na hata milele.

¹¹⁸ Sasa, kwa hiyo mnaona, Mikaya alikuwa—alikuwa amewekea msingi imani yake juu ya ono lake kwanza, kisha akalichukua ono lake na kulilinganisha na Neno la Mungu, ndipo akajua alikuwa sahihi.

¹¹⁹ Na sasa, hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya. Kama—kama theolojia yetu itachukua Neno la Mungu, na ninii yetu, mambo tufanyayo, nayo yanashikamana kote katika Biblia, pamoja kabisa na Biblia, hiyo ni sawa, basi ukifanya hivyo, utakuwa sawa, lakini kama sivyo, achana nalo, Mungu atabariki tu yale aliyosema angeyabariki.

¹²⁰ Sasa, tunaona ya kwamba Ahabu alikuwa ni mtu aliyelaaniwa, kwa sababu nabii, ndipo akasema, “Nilikuwa, ono langu la mwisho,” akasema, wakati alipoona ono, alimwona Mungu ameketi juu ya kiti cha enzi, kisha akasema jeshi la Mbinguni lilikuwa limesimama mkono Wake wa kuume na mkono Wake wa kushoto, na hapana shaka walikuwa na mkutano wa baraza, Naye akasema, “Tunaweza kumtuma nani ashuke aende kule na kumdanganya Ahabu,” sasa, kumbukeni, “kumdanganya Ahabu, na kumleta huko nje kwenye konde lile, apate kuuawa, kutimiza Neno la Eliya?” Utukufu! Haleluya! Jinsi Mungu atakavyosimama nyuma ya Neno Lake!

¹²¹ Huyu alikuwa ni nabii aliyesema hivyo, bali Yesu alisema, “Ukiuambia mlima huu, ‘ng’oka,’ wala usiwe na shaka, bali uamini ya kwamba yale uliyosema yatatimia, yatakuwa yako yale uliyosema,” unapojua ni Neno la Bwana likizungumza.

¹²² Hiyo ndiyo sababu ningeweza kumwambia mwanamke huyo, aliyekuwa na uvimbe mkubwa, kwa yule mama mwenye kansa hapa usiku wa leo, hao mbalimbali, kwa sababu kwanza, ni ono, linalingana na Neno, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Hilo hapo ono, halafu linatukia, ni BWANA ASEMA HIVI, nalo halina budi kutukia. Hakuna kitu kinachoweza kulizuia. Mnaona?

¹²³ Sasa, ilikuwa ni muda mrefu tangu Eliya alipotoa unabii huu. Alikuwa Utukufuni kwa muda mrefu. Lakini angeweza, alikuwa ametoa unabii huu, naye alijua ulikuwa unakuja kutimia. Halafu basi Mikaya alijua ya kwamba Eliya alikuwa ni mtu wa Mungu, na huyu hapa Mungu juu Mbinguni akifanya baraza Kule juu, jinsi ya kulifanya Neno la Eliya litimie.

¹²⁴ Na kama *una* Neno la Bwana, na *utanena* Neno la Bwana, wala usilitilie *shaka* Neno la Bwana, Mungu atafanya mkutano wa baraza kulifanya Neno lako litimie, kwa sababu si neno lako, ni Neno Lake. Ni Neno Lake, kama ni BWANA ASEMA HIVI, kama kweli ni BWANA ASEMA HIVI.

¹²⁵ Angalieni, sasa, walifanya baraza. Na kwa hiyo roho mmoja akatokea, hapana shaka alitoka maeneo ya chini, hapana shaka

aliinama, na kusema, “Mungu, nita—nitaninii, ni—ninajua jinsi tutakavyofanya hilo.”

“Basi, una mpango gani?”

¹²⁶ Kasema, “Nitashuka niende, na kuingia ndani ya hao wahubiri wote, na kuwafanya watabiri uongo, kwa sababu hawayajui Maandiko kwa vyovyote vile,” kwa hiyo akasema, “Nitashuka niende na kuwafanya watabiri uongo. Na kwa hiyo tutamwinua, na kumpeleka huko nje, ndipo basi unaweza kumfanya auliwe huko nje kutimiza Neno la Eliya.”

Kwa hiyo, Yeye akasema, “Utafanya hivyo, wewe ni, utamshawishi.”

¹²⁷ Na kwa hiyo wakati aliposema hivi, sasa unaweza kuwazia jinsi huyo askofu alivyofikiria wakati maskini mhubiri huyo wa asiyethaminiwa, akisimama pale, akitamka neno kama hilo, alienda moja kwa moja na kumpiga kofi moja papo hapo mdomoni, naye akasema, “Roho wa Mungu alienda njia gani aliponiacha?”

Akasema, “Utaona, siku moja, ukiketi kwenye kizimba kule,” kasema.

¹²⁸ Eliya—Eliya alikuwa ametabiri jambo hilo, nalo ono la Mikaya likalingana na Neno la Mungu.

¹²⁹ Sasa, kama imani yako inasema... Sasa, ni wangapi wanaoamini ya kwamba kuna kitu kama uponyaji wa Kiungu kwa Kristo? Inua mkono wako. Vema. Ni wangapi wanaoamini ya kwamba ungeweza kuponywa usiku wa leo? Inua mkono wako. Vema, hu—huo hapo u—ufunuo wako ukilingana na Neno la Mungu, basi hauna budi kutimia. Amina. Yeye—Yeye hana budi kufanya hivyo, kama kweli unaamini. Usijifanye tu kuliadini, sasa, hatadanganya, Shetani hatadanganya, bali huna budi kupata matokeo.

¹³⁰ Siku kumi baada ya Yesu kuwapa wanafunzi uwezo wa kutoa pepo, tunawaona kule wameshindwa na ugonjwa wa kifafa. Nami ninaweza kumwazia mmoja wao, Andrea, akisema, “Sasa, hivi ndivyo nilivyolifanya huko Filipi, hili hapa: Ondoka humo, ewe ibilisi! Ondoka humo, ibilisi!” La, asingetoka.

¹³¹ Petro akasema, “Hamjui jinsi mnavyofanya, hivi ndivyo tulivyolifanya huko Kapernaumu, hebu niwaonyeshe jinsi unavyolifanya: Mshike namna *hii*, useme, ‘Unajua mimi ni nani? Mimi ni Simoni Petro! Ondoka humo!’” Ibilisi akazidi tu kuendelea.

¹³² Kwa hiyo baada ya kitambo kidogo huyo baba akainua macho yake, naye huyu hapa Yesu akaja, akaja akitembea, kasema, “Bwana, nilimleta mtoto wangu kwa watumishi Wako nao hawangeweza kumsaidia kwa vyovyote.”

Kasema, Yesu akasema, “Ninaweza, kama ukiamini.”

Akasema, “Mimi, Bwana, saidia kutokuamini kwangu,” kasema, “Ninaamini.”

133 Wakati Yesu alipoenda akipanda juu, hivyo tu ndivyo alivyopaswa kufanya, huyo ibilisi alijua ya kwamba kulikuwa na kitu Fulani mbali na mwanadamu anayetembea pale, basi. Mnaona?

134 Kwa hiyo basi, sasa baada ya yote kwisha, ibilisi akamwacha huyo mtoto, na baada ya hayo kwisha, ndipo wanafunzi wakamwita Yesu kando na kusema, “Sasa, kwa nini tusingeweza kufanya hivyo? Kwani ulituondolea zile nguvu?”

Akasema, “La.”

135 Ninaweza kuwaonyesha mahali alipowapa zile nguvu, bali siwezi kuwaonyesha mahali alipoziondolea, zingali zipo, mnaogopa tu kuzitumia. Mnaona?

Kasema, “Naam, lakini, kwa nini ha—kwa nini hatukuweza kumtoa?”

136 Yesu akasema, sasa, hakusema, “Kwa sababu nilizichukua zile nguvu tena.” Akasema, “Kwa sababu ya kutokuamini kwenu.” Jambo ndilo hilo. Mnaona? Jambo ndilo hilo. “Kwa sababu hamwamini.”

137 Sasa, Mikaya asingaliweza kuwa na imani pasipo ono lake kulingana na Neno la Mungu. Hivyo ndivyo, katika, nilipokuwa nikizungumza juu ya Ibrahimu na Uzao wake baada yake, jinsi tu nilivyo na imani na hilo ono langu, juu ya hilo, kwamba ni Neno la Mungu hasa. Ndipo, unakuwa na imani: “Ninajua ndivyo *ilivyo*.”

138 Mungu anaposema hivyo, Naye ameliyahidi kwa Neno Lake, nawe unaishi katika siku hii, Yeye anafanya kazi kwa wakati uliopangwa. Naam, bwana. Hakuna kitu kitakachouzia, unaendelea moja kwa moja. Na hiyo ndiyo sababu ninaamini, usiku wa leo, ya kwamba tunaishi katika vivuli vya wakati tu . . .

139 Mhudumu mmoja hapa hivi majuzi, huyo mvulana hayuko hapa usiku wa leo, yeye ni Mbaptisti na alichukua digrii za kila namna, nao, kanisa lake, lilimfukuza, nao watu wake wakampeleka kwenye hospitali ya wendawazimu, yeye na mkewe. Alikuwa hapa jana usiku. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Ninakubaliana na huyo ndugu kabisa.

140 Na kile linachofanya, haliyafikii yale makanisa makubwa mno, linashuka moja kwa moja chini, kama vile Yesu alivyofanya, kama manabii walivyofanya, kama hao wengine wa ninii, siku zote moja kwa moja, ni kwa watu maskini, na linatukia, limekwisha, ndipo wanasema, “Vema, ilikuwaje? Si—sikujuu hilo.” Hakika. Yeye huwafunulia wale wanaomtazamia, wale watakaoketi kimya na kuusikiliza kwa dakika moja, na kuyararulia mbali mawazo yako mwenyewe, na kulinganisha yale unayosikiliza kwenye Neno la Mungu.

141 Sasa, kama Ahabu angaliketi chini kwa dakika moja, ama kama kuhani mkuu huyo, ama yeyote wa hao manabii, angeketi chini na kulinganisha, si kile kilichoonekana sawa, ilionekana kana kwamba hiyo ilikuwa ni mali ya Israeli, bali si jinsi linavyoonekana, ni kile Mungu alichosema kulihusu, mnaona. Laiti wangaliketi chini na kulilinganisha!

142 Inaonekana kana kwamba tunapaswa kuchukua na kuwa na shule zetu na makanisa ye—yetu ya *juu* sana, yenye Ph.D. na LL.D., nasi tunapaswa kuwa na majengo makubwa kuliko yote, mazuri kuliko yote ulimwenguni, na tunapaswa kufanya huku—huku kusoma kwote, kuandika, na hesabu. Lakini hivyo sivyo Mungu alivyosema, Yeye kamwe hakusema enendeni mkawaelimishe watu. Hilo ni sawa. Siungi mkono ujinga wangu sasa kwa eli-. . . au—au kuutumia huo kama gongo. Lakini angalieni, ninasema hivi: Elimu ni sawa, bali kamwe haitachukua mahali pa wokovu. Mnaona?

143 Loo, michezo ya mpira, na—na mizaha, na kadhalika, hiyo ni sawa, bali si mali ya kanisa. Kanisani tunamtaka Kristo, si mfano wa Kristo, wala picha ya Kristo, ama Kristo aliyekufa, ama kaburi la Kristo, tunamtaka Kristo *aliyefufuka*, aliye hai pamoja nasi, akijithibitisha Mwenyewe ya kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Hilo ndilo Kanisa litakalo, lile wanalopaswa kutamani, inategemea hamu ya chakula ilivyo, mnaona, na kama watalipokea au la.

144 Sasa, alilinganisha ono lake, basi, na yale Neno la Mungu liliyosema, ndipo akasimama pale pale mbele ya hayo mataifa mawili na kuwaambia, akasema, “Hutarudi, utafia uwanjani.”

145 Nanyi mnajua Ahabu alisema nini? Kasema, “Mrudishe jamaa huyu, na mumwambie meya wa jiji amfunge gerezani, akamlishe chakula cha huzuni na maji ya shida, nami nitakaporudi kwa amani,” kasema, “Ni—ni—nitamshughulikia nitakaporudi.

146 Mnajua yale Mikaya aliyosema? Aligeuka, akamtazama, akasema, “Na kama ukirudi kamwe, Bwana hakusema nami.” Loo, alijua mahali alipokuwa amesimama. Hivyo ndivyo mtu yeyote angefanya.

147 Hivyo ndivyo maskini mama huyo alivyofanya kuhusu mtoto wake mchanga, wakati alipokuwa na *hakika* sana kama ningemwombea! Hivyo ndivyo yule mama mwenye uvimbe mkubwa kule nyuma, amelala kule nyuma! Haidhuru ilimbidi kufanya nini, kulima kote, kupitia kwenye paa ama popote pale, kusudi tu aweze kufika kule, hilo tu ndilo alilotaka, kwa kuwa ilikuwa ni imani yake, ililinganishwa na Neno la Mungu, naye alijua ya kwamba Yesu Kristo alikuwa angali hai, kwa hiyo alikuwa na imani, na likafanyika.

148 Sasa, sasa tunaona ya kwamba—ya kwamba Mi-. . . ya kwamba kila kitu ambacho Mika alikuwa amesema, ama,

Mikaya alisema kilitimia hasa. Na kila nabii kote katika nyakati (Sasa tunafunga.), kote katika wakati, aliyewahi kufanya lolote na Mungu, alichukua msimamo wa Neno la Mungu. Sasa, hawakuondoka kwenye Neno, haidhuru hali ya mambo ilionekanaje, hawakuondoka kwenye Neno.

¹⁴⁹ Nuhu, Mungu alimwambia Nuhu itanyesha, Nuhu hakuondoka kwenye hilo, alidumu moja kwa moja nalo, haidhuru, labda sayansi, ambayo walikuwa nayo kubwa wakati huo kuliko waliyo nayo sasa, kwa hiyo waliweza kujenga vitu na kufanya mambo wakati huo, hatuwezi kuyafanya sasa, katika—katika—katika sayansi ya ulimwengu huu, walijenga piramidi na Sfiniksi, na kadhalika, ambazo tusingeweza kujenga kama hizo.

Lakini akasema, “Kwani hiyo mvua inatoka wapi?”

¹⁵⁰ Nuhu asingeweza kuwaambia hilo, asingeweza kujibu swali lao, lakini alijua Mungu alikuwa amesema naye, kwa hiyo alikuwa akidumu moja kwa moja pamoja na Neno, akasema, “Mungu alisema hivyo.” Mnaona?

¹⁵¹ Ibrahimu asingeweza kusema, wakati alipokuwa na umri wa miaka mia moja, jinsi atakavyompata mtoto kwa Sara, naye tisini.

¹⁵² “Utawezaje . . . ? Vipi . . . ? Nithibitishie. Hapa, yeye—yeye ni mkongwe, tumbo lake la uzazi limekauka likaiisha. Mbona, ninyi nyote hata hamjawa na uhusiano wa familia kwa miaka ishirini, nawe huyu hapa, wasema utampata mtoto. Utampataje?”

“Sijui.”

“Vema, unajuaje utampata?”

¹⁵³ “Mungu alisema hivyo.” Sasa, hilo latosha. Dumu moja kwa moja na Neno. Manabii wote wa kweli hudumu na Neno. Wakati mwingine linawaingiza katika shida, karibu wakati wote, linawaingiza, bali Hilo—bali Hi—Hilo sikuzote ni la kweli.

¹⁵⁴ Wale wana wa Kiebrania walisema, “Mungu wetu anaweza kutochoka na tanuru hiyo ya moto, bali hatutasujudu kitu kingine chuchoke, hilo ni jambo moja, hakika, afadhali tuteketee kuliko kulighairi.” Kwa hiyo iliwagharimu saa chache za maombi usiku mmoja, kisha wakashushwa kwenye tanuru iliyowaka moto kesho yake asubuhi, lakini walikuwa na maongezi na Mtu kama Mwana wa Mungu aliyesimama mle ndani. Mnaona? Lakini walidumu pamoja na Neno.

¹⁵⁵ Danieli alisema, “Sijali mnatoa matangazo mangapi, nina tabia ya kwenda dirishani na kufungua dirisha kuelekea mashariki na kumwomba Mungu wangu.” Ilimgharimu usiku kucha katika tundu la simba, bali alidumu na Neno, hiyo ni kweli, a—akatoka. Mungu daima hulishughulikia Neno Lake. Naam.

¹⁵⁶ Daudi wakati alipokuwa huko juu wakati huo mbele ya Sauli, alimsikia maskini yule Goliathi mkubwa akija pale na kusema, “Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama hicho.” Mnaona? Ah, la, hilo lilikuwa toleo lake la 1961, samahani, nitarudi nyuma. Alisema, “Hebu baadhi yenu mje hapa mkapigane nami,” mnaona. Kwa hiyo akasema . . .

¹⁵⁷ Naye Sauli, tangu mabega kwenda juu alikuwa juu ya jeshi lake, na huko juu, basi akasema, “Vema,” akasema, “Nitakwambia, ni jambo baya, mtu huyo, jamani, ataninii . . . angalia angekuwa na uzito gani, naye ana ninii . . . mbona, vidole vyake vina urefu wa inchi kumi na nne.” Kasema, “Vema, nini . . .?” Hivyo ndivyo Biblia isemavyo. Naye alikuwa na m—mkuki kama sindano ya mfumaji, ambao labda ungevuka upande wa pili wa chumba *kile*. Naye akasema, “Mbona, ni nani angeweza kupanda kule na kupigana na jamaa kama huyo?”

¹⁵⁸ Ndipo huyu hapa akaja maskini nanii mdogo . . . Nalo jeshi lote likarudi nyuma, Waisraeli, mwajua, wanaodhaniwa kuwa ni watu wanaomcha Mungu, wakarudi nyuma, kasema, “Loo, jamani! Loo, hatuwezi kufanya hivyo, jamani, hakuna mtu atakayemgusa jamaa huyo.”

¹⁵⁹ Akasema, “Hebu niwaambie nitakalofanya, hakuna haja ya kumwaga damu nyingi kupita kiasi,” kasema, “mmoja wenu tu na aje hapa, akapigane nami, na yeyote yule, kama mkiniua, basi majeshi yetu, tutawatumikia.” Mnaona, hivyo ndivyo ibilisi anavyopenda kujigamba anapofikiri anaweza kukushinda. Unaona?

¹⁶⁰ Kwa hiyo siku moja akasema hivyo wakati mmoja mara nyingi zaidi, kulikuwa na maskini jamaa mdogo amesimama pale, kidogo, labda ameinama mabega, maskini mtoto mdogo, amejifunga ngozi ya kondoo namna *hiyo*, na kombeo mkononi mwake.

¹⁶¹ Ndipo Goliathi akatokea na kusema, “Ninyi nyote huko mnaodai kuwa Wakristo, mwajua, *fulani-na-fulani-na-fulani*, vema, njoni huku na hebu tuone hili,” akasema, mnaona.

Daudi akasema, “Mnataka kuniambia ya kwamba mtasimama hapo na kumwacha Mfilisti huyo asiyetahiriwa ayatukane majeshi ya Mungu aliye hai?”

¹⁶² Ndipo ndugu yake akasema, “Sasa, unakuwa mtukutu, nitakushtaki kwa Baba utakapoenda nyumbani, unaona, hilo tu ndilo nitakalofanya, sasa, unajaribu kujionyesha.”

Kasema, “Sijionyeshi, lakini kuna jambo la dharura hapa,” kasema, “kuna jambo fulani hapa, huyo mtu anayatumkana majeshi ya Mungu aliye hai.”

¹⁶³ Kwa hiyo wakampeleka kwa Sauli, nami ninawazia Sauli akisema, “Ninapendezwa na ujasiri wako, mwanangu, lakini,” kasema, “loo, jamani,” kasema, “mbona, wewe si kitu ila mtoto

mchanga, naye amekuwa mpi—amekuwa mpiganaji tangu ujana wake. Hujuu jinsi ya kutumia upanga wala chochote.”

¹⁶⁴ Akasema, “Lakini mimi, angalia,” akasema, “Nina ujuzi fulani niliopata wakati mmoja, simba aliingia,” kasema, “Mimi huchunga kondoo, basi simba aliingia, akamkamata mmoja wa kondoo wa baba yangu, nami ni—ni—ni—nikamwua.” Kisha kasema, “Halafu dubu akaingia na kumchukua mmoja, nikamwua.” Ndipo kasema, “Basi ni zaidi sana vipi Mungu atanipa Mfilisti huyo asiyetahiriwa!” Mnaona? Kasema, “Si—simba alichukua mmoja wa kondoo wa baba yangu na kutoka mbio,” kisha kasema, “basi alipofanya hivyo, nilimfuatilia kondoo huyo na kumrudisha.” Ninapenda ujasiri huo, nanyi je?

¹⁶⁵ Mnajua nini? Kuna wengi wenu ninyi kondoo huko nje, hamna simba, bali kansa, ama uvimbe, ama ibilisi fulani alikunyakua na kukimbia. Tunakuja usiku wa leo, hiyo ni kweli, tukiwarudisha kondoo wa Baba, wewe kuwa tayari kujisalimisha. Kristo wa Mungu yuko hapa, Yeye atakurudisha moja kwa moja kwenye afya tena. Ugonjwa au mateso yamekupata, jana usiku, kwenye viti vya magurudumu, na kadhalika, chochote kile, unaona, mateso yanakuchukua, bali Baba yuko hapa kukukomboza, Roho Mtakatifu. Daudi alisema . . .

¹⁶⁶ “Loo,” kasema, “sasa itakubidi kupata mafunzo ya kitheolojia kabla hujaenda huko nje kufanya hivyo,” unajua. Kwa hiyo akasema, “Afadhali uchukue tu utaalamu wangu ili uninii . . .” Kwa hiyo akamvika silaha zake kubwa namna *hiyo*, naye maskini Daudi akaanguka mpaka chini. Alikuta kwamba fulana ya kikanisa ya Sauli haikumwenea mtu wa Mungu, kwa hiyo hakutaka makaratasi yoyote yake ya kimadhehebu.

¹⁶⁷ Kwa hiyo akasema, “Niondolee kitu hicho, sijawahi kukithibitisha, sijui lolote kukihusu, bali ninajua kuhusu *hili*,” akasema, “niache niende na kile ninachokiamini.” Ndipo akachukua kombeo hilo dogo akaenda huko nje, ndipo Mungu akalielekeza jiwe hilo na kuliua jitu hilo. Kwa nini? Alidumu na Mungu, alidumu kwenye imani yake. Kweli. Kila nanii wa kweli . . .

¹⁶⁸ Petro na Yohana, walipopitia kwenye lango liitwalo Zuri, wakiagizwa na Mungu kwenda kuwaombea wagonjwa, hapo palikuwapo na mtu aliyekuwa kiwete tangu tumboni mwa mamaye, akasema, “Sina fedha wala dhahabu, lakini nilicho nacho nakupa.”

Kasema, “Una nini?”

“Nina imani katika Yesu Kristo. Unayo iyo hiyo?”

“Naam, bwana.”

¹⁶⁹ “Simama kwa miguu yako basi.” Amina. Haya basi. Walimwinua tu basi, alikuwa akitetemeka na kuyumbayumba,

wakaendelea tu kumshikilia, moja kwa moja akaanza kupata nafuu kidogo, huyu hapa akaenda, akitembea moja kwa moja. Akalishikilia, alidumu na agizo Lake, akadumu na Neno.

¹⁷⁰ Yesu, wakati alipokuwa hapa duniani, aliye mkuu kuliko wote, hakujakuwako na mmoja kama Yeye, na kamwe hakutakuwako, lakini wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, Yeye alidumu na Neno, alimshinda ibilisi kwa Neno la Mungu. Ibilisi akasema, alikuwa akimjaribu, kasema, “Mbona, unajua imeandikwa, sasa . . .”

Akasema, “Naam, na pia imeandikwa!”

Akasema, “Vema, unajua mimi ni mwanatheolojia.”

Akasema, “Naam, nami, pia.”

Kasema, “Vema, i—imeandikwa atawaagizia Malaika Wake juu Yako usije wakati wowote, ukajikwaa kidole . . .”

“Naam,” Yeye akasema, “pia imeandikwa, usimjaribu Bwana Mungu Wako. Kwa hiyo rudi nyuma Yangu.” Huyu hapa akaenda zake. Mnaona?

¹⁷¹ Neno la Mungu, manabii wote wa kweli, Wakristo wote wa kweli, waaminio wote wa kweli, hudumu na Neno hilo, haidhuru mtu yeyote anasema nini, unadumu moja kwa moja na Neno. Wanasema siku za miujiza zimepita, usiamini hilo, kwa kuwa Biblia ilisema ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

“Vema,” unasema, “tunaamini hilo.”

¹⁷² Vema, kama Yeye ni yule yule, basi atatenda vile vile, atafanya vile vile. Hiyo ni . . .? Ingenifaa nini, kusimama hapa na kuhubiri hayo, kama Mungu asingeshuka na kusema ndivyo ilivyo? Sasa, huwezi kusema si Neno la Mungu, kwa hiyo ni Neno la Mungu, huu hapa ushahidi wa wengine ambao wamelithibitisha.

Unaamini usiku wa leo kwa moyo wako wote? Unaamini kwa moyo wako wote? Hebu na tuinamishe vichwa vyetu, basi, kwa muda kidogo tu.

¹⁷³ Baba yetu wa Mbinguni, sasa hivi nimefungua kurasa za Biblia, Hiyo ndiyo Neno lililoandikwa, sasa tunataka Neno lililofanyika mwili na kukaa kwetu, jalia ashuke aje sasa mwenyewe, na kutuonyesha wema Wake na rehema Yake, jalia atuonyeshe kufufuka Kwake, jalia aonyeshe nguvu Zake ya kwamba Yeye angali ni yeye yule.

¹⁷⁴ Sasa, sisi ni watu wadogo tu, watu wanaoteswa, wanaochekwa, na hivyo ndivyo imekuwa daima. Nasi tunapenda kusimama pamoja na Paulo usiku wa leo na kusema, “Njia waliyoiita uzushi, kichaa, hivyo ndivyo ninavyomwabudu Mungu wa baba zetu.”

¹⁷⁵ Na sasa, Bwana, tunaishi katika siku hii kuu, ambayo imetabiriwa, ya kutokuamini kila upande. Tunako kwa wingi,

ulimwengu umesongwa nako kabisa katika Wakati huu wa Kanisa la Laodikia.

¹⁷⁶ Hata wakati kanisa Lako Mwenyewe limechukizwa Nawe, na kurudi nyuma, na kukimbilia mambo ya ulimwengu, kanisa lingekuwa bora zaidi kama Yesu angalikuja kulichukua miaka arobaini iliyopita, kuliko lilivyo usiku wa leo, maana yote yamevunjika-vunjika katika hali ya kila namna na mapokeo.

¹⁷⁷ Na wahudumu wachanga wakiinuka kutoka kwenye seminari pamoja na akili zao na kadhalika, na pasipo kuijali Biblia huku wakichukua mapokeo, na kadhalika, nao wameichafua kabisa kama tu walivyofanya sikuzote.

¹⁷⁸ Mungu, ungali unabaki yeye yule, kama tu ulivyofanya, huko nyuma katika siku za—za manabii, Wewe ni Mungu yeye yule leo. Ninaomba, Baba, ya kwamba utajidhihirisha Mwenyewe kuwafanya watu wajue.

¹⁷⁹ Sasa, kuhubiri, ulimwengu umehubiriwa ukaingizwa kwenye mauti, maskini watu hawajui la kuamini, wanakimbia *hapa* na *pale*. Kama tu ulivyosema, katika siku za mwisho kutakuja njaa, si ya mkate tu, bali ya kusikia Neno la kweli la Mungu, na kwamba wakati *huo* umekaribia sasa, Bwana, ulisema wangeenda mashariki na magharibi, kaskazini na kusini, wakitafta Neno la Mungu.

¹⁸⁰ Sasa, Baba, kweli ndivyo ilivyo sasa, twasikia watu wakisema wangetembea maili thelathini juu ya mawe, miguu mitupu, wapate kuingia katika mkutano mwingine mzuri wa kiroho kama walivyokuwa nao miaka arobaini iliyopita. Lakini, Ee Mungu, wanaupata wapi? Wanaingia katika lundo la mafundisho ya sharti ya kujibunia.

¹⁸¹ Lakini, Bwana, Wewe uliahidi itakuwa hivyo. Tulikuona Wewe katika Wakati huo wa Kanisa la Laodikia, ulisukumwa nje ya kanisa Lako, wakati pekee waliokutoa nje ya kanisa Lako Mwenyewe, Nawe ulikuwa ukibisha mlangoni, “Mtu akiona kiu, nitafungua na kuingia.”

¹⁸² Baba, ninaomba ya kwamba kutakuwa na watu wengi wenye kiu hapa usiku wa leo, watakaona kiu, “Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana watashibishwa.”

¹⁸³ Sasa, sisi, kama Kanisa Lako, tunajisalimisha Kwako, naomba utushughulikie kama watoto Wako, tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁸⁴ Billy yuko wapi? Je, kulikuwa na kadi za maombi zilizosambazwa leo? Au alisambaza? Vema, hebu tusizitumie. Hebu na tumwache Mungu awe Kadi yako ya Maombi, usiku wa leo. Ninajisikia tu kuongozwa kufanya jambo hili. Kabla sisi. . . Naam, hivi ni vitambaa ambavyo tunaomba kulingana na Matendo 19, 19:11, tunaona.

185 Sasa, ni wangapi hapa wasio na kadi ya maombi? Inueni mikono yenu, hamna kadi za maombi nanyi ni wagonjwa? Vema, ni wangapi walio na kadi za maombi basi? Inua mkono wako. Loo, jamani! Moja, mbili, nadhani hakuna zaidi ya thelathini walio na kadi za maombi, na yapata mia tatu walio wagonjwa. Vema, kwa hiyo walio wengi wako upande huo mwingine. Hebu na tushikilie tu hizo kadi za maombi mpaka usiku mwingine.

186 Hebu tuseme tu hivi: Kama Mungu akidumu Mungu, na samahani kwa kutoa tamshi hilo la kukufuru, Mungu *ni* Mungu, na kama Yeye ni Mungu, Neno Lake lingali ni lile lile, na Biblia inasema ya kwamba kwa kupigwa Kwake mliponywa. Kama Bwana Yesu huyo angekuja usiku wa leo, ambapo, Yeye angekuja, ingekuwa ni mwisho wa wakati, tunajua hilo, lakini kama angeonekana hapa, usiku wa leo, naye angekuwa amesimama hapa kwenye jukwaa hili, kama mnavyoniona nimesimama, nawe umjie na kusema, “Bwana, utaniponya?” Asingeweza kufanya hivyo, angekuwa akiasi sheria Yake mwenyewe.

187 Mnaona, Yeye angesema, “*Tayari* nimekuponya.” Kwa kupigwa Kwake sisi *tuliponywa*. Huenda kwa namna fulani akakukemea kwa kutokuamini, lakini ange—angeninii, kwa kupigwa Kwake *uliponywa*.

188 Sasa, ni wangapi wamekuwa hapa na kunisikia nikihubiri Jumapili iliyopita alasiri juu ya Uzao wa Ibrahimu, na jinsi ambavyo, uh, mmesikia, na kadhalika?

189 Sasa, wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, hebu tuone tu kile alichokuwa hapa duniani. Wakati alipokuwa hapa duniani, alikuwa na mistari ya maombi, nadhani, hakika, lakini mara nyingi Yeye alisimama, akaangalia huko nje juu ya kusanyiko, na kuwapambanua watu. Hiyo ni kweli?

190 Ni wangapi wanaojua kwa kusoma Maandiko hiyo ilikuwa ni ishara Yake ya Masihi? Ni wasomaji wangapi wa Maandiko, wa Biblia wanajua hilo? Unataka kusema kuna *idadi hiyo* tu ya wasomaji wa Biblia hapa ndani usiku wa leo wanaojua hilo? Karibu theluthi moja ya watu waliinua mkono wao. Ni Wapentekoste wangapi walio hapa ndani, usiku wa leo? Inua mkono wako. Aibu kwenu au mchungaji wenu, mmojawapo! Kwani hamjui ishara ya Masihi ilikuwa nini?

191 Musa alisema Masihi atakuwa nini? “Bwana Mungu wenu atawaondokeshea...” mwalimu? “...Nabii, kama nilivyo mimi.”

192 Basi walipoona...Naye Mungu alisema, “Akiwepo nabii, naye anafanya ishara ya nabii, nayo inatimia, basi mwaminini, kwa sababu Mimi—Mimi, Mimi, hilo ni Neno Langu, lakini lisipotimia, basi msimwamini.”

193 Sasa, wakati Yesu alipokuwa duniani, jinsi alivyojithibitisha Mwenyewe kuwa Masihi, sasa, ninataka kuwaonyesha baadhi

yenu Wapentekoste jambo hili: Mwangalieni yule mwanamke Msamaria, sasa, muda wote ambao mmekuwa katika Pentekoste, hata hivyo mwanamke huyo Msamaria mwenye sifa mbaya alijua mengi zaidi kuhusu Biblia alipomwona Yesu, kuliko mnavyojua, maana wakati Yesu alipozungumza naye na kusema, “Mwanamke, nenda kamwite mumeo”:

Alisema, “Sina yeyote.”

Akasema, uh, Yeye akasema, “Hiyo ni kweli, una, ulikuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye wako, kwa hiyo umesema kweli.”

¹⁹⁴ Naye akasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii. Tunajua ajapo Masihi, Yeye atatwambia mambo hayo.” Alijua hiyo ingekuwa ndiyo ishara ya Masihi. Mnaona?

Naye akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

¹⁹⁵ Akakimbia mjini, akasema, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyofanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?” Nayo Biblia ilisema ya kwamba mji huo wote ulimwamini Yesu kwa sababu kwamba, uh, ya neno la mwanamke huyo. Sasa, ni wangapi wanaojua hiyo ni kweli? Mnaona?

¹⁹⁶ Vema, kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi jana, basi Yeye. . . Huwezi kupata Andiko moja ambapo alifanya hivyo mbele ya Mata- . . . , uh, kwa Mataifa, sasa, maana Injili ilikuwa bado haijawaendea Mataifa. Lakini Yeye aliahidi ya kwamba kab- . . . mwishoni mwa wakati wa Mataifa, wakati Mataifa sasa wanamtazamia Masihi. . . Hivi tunamtazamia? Vema, basi, kama akitokea katika umbo tofauti na alivyoonekana wakati huo, basi si Masihi yeye yule. Kwa hiyo hana budi kuja kwa Mataifa katika jambo lile lile, naye Yesu alisema angekuja, kasema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.”

¹⁹⁷ Nasi tunaona ya kwamba wakati Bwana aliposhuka katika mwili wa kibinadamu mbele ya Ibrahimu, Kanisa teule, wakati Billy Graham wa kisasa na hao wengine waliposhuka na kuhubiri huko chini Sodoma, kumtoa Lutu, na kanisa kule chini, nje, bali kwa kundi teule, huyo Malaika aliketi huku ameelekeza mgongo Wake kwenye hema na kusema yale Sara aliyokuwa akifanya ndani ya hema. Hiyo ni kweli? Naye Yesu alisema jambo lilo hilo lingetukia kabla tu ya kuja kwa Mwana wa Adamu.

¹⁹⁸ Sasa, msiwe mkizunguka-zunguka, ketini kimya na mwe na kicho. Ni wangapi huko nje wanaoamini ya kwamba Yeye angali ni Mungu yeye yule? Vema, ninyi ombeni, iweni tu na imani, msitie shaka, ombeni.

¹⁹⁹ Na sasa, mbele za Mungu Mwenyezi, aliye Hakimu wangu, kwa kusanyiko hili la watu, walionunuliwa kwa Damu Yake, nitaona kama kuna mtu yeyote hapaa ambaye kwa kweli

ninamjua humu jengoni. Sasa, kama sijakosea, papa hapa upande huu, mtu huyu aliyeketi hapa, yeye na mke wake, nafikiri ninawajua watu hao. Hiyo ni kweli, bwana? Nami na—nafikiri huyu ni ndugu yetu wa thamani ambaye daima huleta maua hapa, na huyo mama aliyeketi hapo mwisho, nafikiri ninawajua. Na moja kwa moja huko nyuma kuna marafiki zangu wema, hao wawili wanaofuata hapo nyuma, ni Ndugu na Dada Dauch kutoka huko Ohio. Hiyo si ni kweli? Hivi huyo ni wewe, Dada Dauch, na Ndugu Dauch?

²⁰⁰ Sasa, nyuma huko chini sioni mtu yeyote, na kupitia hapa. Huyu si ni Ndugu Stricker aliyeketi papa hapa mbele, sivyo? Papa hapa amevaa shati la manjano? Ni nani wako...? La. Nami ninajua Ndugu Stricker yuko hapa mahali fulani, kwa sababu nimemwona leo, lakini sijui mahali alipo, na, loo, naam, huko nyuma kabisa pembeni, huko nyuma kabisa. Vema, kuona tu, na—nadhani hao ndio wote niwajua kwenye kusanyiko.

²⁰¹ Sasa, wewe omba, na uamini, na useme hivi: “Bwana Yesu, ninajua ya kwamba nani, mtu huyo hapo juu ni mwanadamu tu,” mnaona, “lakini ninaamini ya kwamba tunaishi katika siku za mwisho. Nami huyu hapa nimeketi hapa nami ni mgonjwa, nayo Biblia inaniambia ya kwamba Wewe ni Kuhani Mkuu ninayeweza kumgusa kwa mambo ya udhaifu wangu.” Ninyi nyote mtakubaliana na jambo hilo? Hiyo ni Biblia.

²⁰² Vema, basi, wakati huyo Kuhani Mkuu alipokuwa hapa duniani, mwanamke, siku moja, aligusa vazi Lake, naye akasema, “Nikiligusa tu vazi Lake, nitakuwa mzima.” Kwa hiyo akamgusa, kisha akaondoka, akaketi chini, labda kama ulivyo hapo, ama alisimama, vyovyote ilivyokuwa.

²⁰³ Yesu akageuka, akasema, “Ni nani aliyenigusa? Ni nani aliyenigusa?” Ndipo Petro akamkemea na kusema kila mtu alikuwa akimgusa. Lakini Yeye alisema, “Naona nimekuwa dhaifu, nguvu zimenitoka.” Naye akaangalia kote katika kusanyiko mpaka akamwona huyo mwanamke, na kumwambia kuhusu kutokwa kwake na damu, kisha akamwambia, imani yake ilikuwa imemwoko. Hiyo ni kweli? Ni wangapi wanaojua Yesu alifanya hivyo? Semeni, “Amina.”

²⁰⁴ Vema, ni wangapi wanaojua Biblia ilisema ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Amina. Halafu, Biblia ilisema ya kwamba sasa hivi, kwenye wakati huu, Yeye ni Kuhani wenu Mkuu, ameketi mkono wa kuume wa Ukuu, akifanya maombezi mnapokiri, na ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa, sasa hivi, na mambo ya udhaifu wenu. Semeni, “Amina.” Vema.

²⁰⁵ Sasa, wewe ninii tu, ninajisalimisha, ni karama, naam, bwana, karama ya Mungu, wala haitafanikiwa bila ninyi, ninyi ndio mnaopaswa kuwa na imani.

²⁰⁶ Angalieni, yule Mrumi aliyemfunga kitambaa usoni Mwake, kisha akachukua fimbo, na kumpiga nayo kichwani nyuani

asubuhi ile, na kusema, “Kama wewe ni nabii, tuambie ni nani aliyekupiga,” Yesu kamwe hakufungua kinywa Chake, hakuhihi nguvu hata kidogo, askari huyo wa Kirumi hakuhihi.

²⁰⁷ Yesu akisimama pale, ametemewa mate kote usoni Mwake na ndevuni, akitokwa na damu, amefungwa kitambaa usoni Mwake namna *hii*, huku askari wa Kirumi amesimama pale, nusu mlevi, labda, akiwa na mwanzi, kasema, “Aisee, wananiambia wewe ni nabii, unaweza kutambua mawazo ya moyo, tuambie ni nani aliyekupiga, niambie ni nani aliyekupiga, nami nitakuamini,” Yeye hakufanya kitu.

²⁰⁸ Wakati Shetani aliposema, “Kama wewe ni Mwana wa Mungu, fanya mwujiza papa hapa, hebu nikuone ukiufanya, hebu nikuone ukiufanya, ukifanya mwujiza, nitakuamini.”

Akasema, “Rudi nyuma Yangu, Shetani!”

Mmewasikia, hata leo, wakisema, “Hebu—hebu niwaone hawa waponyaji wa Kiungu wakifanya *hivi*.” Mbona, hakika. Bila shaka.

“Rudi nyuma Yangu, Shetani!”

²⁰⁹ Yesu angali yuko. Tunaendelea kumwangalia Yesu, sio wakosoaji, Yesu. Ukielekeza macho yako kwa Kristo—kwa Kristo, hutawaona wakosoaji, endelea tu kusonga mbele. Ninajua Yeye ni yeye yule, kwangu mimi, Yeye ni Mungu wangu, hiyo ni kweli, Mwokozi wangu.

²¹⁰ Sasa, ninyi ombeni, ninyi huko nje, na hebu tuone. Kama atafanya jambo lile lile, kwenu nyote wageni, hapa usiku wa leo, ambao hamjawahi kuwa mikutanoni hapo kabla, itawafanya mwamini? Inueni mikono yenu na kusema, “Ni—ninaamini.” Yapata mikono mitatu.

²¹¹ Hiyo ndiyo sababu Marekani iko katika kuokota masazo yake. Kulikuwa na karibu theluthi mbili ya umati waliosema muda mfupi uliopita walikuwa wageni, nikasema, “Ni wangapi watakoamini, kama Kristo ataonekana hapa na kufanya jambo lile lile alilofanya alipokuwa hai?” Mikono mitatu iliinuliwa. Sasa, mnaweza kuona ni kwa nini hizo kanda, na yale nabii zinayosema. Mnaona? Vema. Ninyi waaminio halisi hata hivyo, anzeni kuamini, anzeni kuwazia, anzeni kuomba.

Inanifanya niseme mambo nisiyotaka kusema, na inanisumbua. (Hebu kidogo, tafadhali.)

²¹² Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba Wewe utakuwa mwenye rehema, Mungu. Si—sijui, labda kama—kama si mapenzi Yako, basi, bila shaka, Baba, halitatukia. Lakini ninaomba ya kwamba utalijalia, ili watu hawa waweze kujua ya kwamba nimenena habari Zako, Wewe nena kwamba ninasema kweli, Bwana, iruhusu irudi. Ninajua Wewe upo hapa, mbona, bila tashwishi yoyote, Bwana, ninajua Wewe uko papa hapa, nami naomba ya kwamba utatujalia.

213 Nimekuwa nikihubiri kwa nguvu, na kuwakemea watu, na kuwaambia juu ya kutokuamini kwao, nao, haidhuru wanaenda kanisani kiasi gani, na wanaimba kiasi gani, wanacheza dansi kiasi gani, na chochote walichofanya, Bwana, isipokuwa wawe waaminio wame—wamepotea. Nami naomba, Bwana, ya kwamba utajalia huo ujulikane, ukweli usiku wa leo, kutokuamini ndiyo dhambi pekee tuliyo nayo, nami naomba, Baba, ya kwamba Wewe utafanya ijulikane.

214 Naomba wasiitumainie haki yao wenyewe. Hao Mafarisayo na makuhani walikuwa wenye haki kadiri walivyoweza kuwa, kwa hiyo hawakufanya chochote kiovu, wasingezungumza neno baya, wasingemkaripia mtu yeyote, wala chochote kile, nawe ukawaambia walikuwa wa baba yao ibilisi, kwa sababu hawakukuamini Wewe, nao walijua Wewe ulikuwa ndiye Masihi.

215 Na, Baba, kwa jambo hilo, tukimwona Roho wako yeye yule akija na kufanya jambo hilo usiku wa leo, nasema jambo lile lile kwa sauti kuu. Simama karibu nami, Bwana, mimi ni mtumishi Wako, katika Jina la Yesu, ninajikabidhi Kwako pamoja na kusanyiko hili. Pitia kwenye kusanyiko hili, Bwana, na uwachague pale, wape imani na uwajalie wakuguse Wewe usiku wa leo, kwa magonjwa yao na shida zao, unathibitisha ya kwamba Wewe ni Mungu, basi nena, Bwana, tunakungojea Wewe, katika Jina la Yesu. Amina.

216 Ninajua Yeye yupo hapa. Asante, Bwana. Mtu huyo aliyeketi hapa kwenye mkono wangu wa kulia, mtu mweusi, aliyeketi hapo, akiomba, mwishoni mwa hicho kiti, utaamini kwa moyo wako wote, bwana?

217 Mwanamke huyo aliyeketi hapo nyuma mwenye kisukari, aliyeketi papo hapo, wa pili hapo ndani, anayeniangalia, unaamini ya kwamba Mungu atakupa afya na kukuponya kisukari? Uliyeketi papa hapa, ukiniangalia moja kwa moja? Kama utaamini, unaweza kuupokea.

218 Vipi kukuhusu wewe, Kasisi? Unawazia nini juu yake? Unafikiri kwamba Mungu atafanya, atakuondolea matatizo hayo ya kiroho na kukufanya uamini? Vema, unaweza kupata kile ulichoomba, basi. Mungu akubariki.

Aligusa nini?

219 Mama huyu aliyeketi, kwangu mimi, papa hapa mwishoni mwa safu, mama mweusi, uliyeketi moja kwa moja hapo, ukiwa na kansa, unafikiri Mungu atakuponya, mama? Una kadi ya maombi? Huhitaji moja. Umeponywa.

Ulipaswa kujibu papo hapo, mama. Uliukosa.

220 Hapa, kwa namna fulani ni mwanamke mnene, aliyeketi papa hapa, akiniangalia, papa hapa chini, amevaa miwani, amezichanua nywele nyuma, ana shida ya kike, ameketi hapo akiomba, unaamini Mungu atakuponya, mama? Unaamini kwa

moyo wako wote? Una ninii yako . . . Una kadi ya maombi? Vema, haitakubidi kuitumia, imani yako ilikuponya.

Nitageuza mgongo wangu. Ninyi ombeni, upande huu.

Kuna mama aliyeketi papa hapa nyuma ambaye ana ugonjwa wa moyo, pia ana yabisi kavu. Papa hapa. Bibi Brady, simama. Simajui mama huyo.

Lakini wanaukosa. Kuna shida gani na huko kutokuamini humu ndani usiku wa leo? Jioneni aibu!

²²¹ Hapa, moja kwa moja kwenye safu kutoka kwa huyo mama, yapata mama mmoja, wawili, watatu, wanne, mama aliyeketi hapo ana vipindi vya udhaifu, ambavyo . . . usiukose, dada. Bibi Rice, simama na ukubali uponyaji wako. Amina.

Unaamini kwa moyo wako wote?

²²² Huyu hapa mama ameketi hapa katika hali ya kufa akiwa na kansa. Bibi Skelton, utaamini kwa moyo wako wote? Simama na upokee uponyaji wako katika Jina la Yesu Kristo. Sasa, ikiwa sikujui, mama, pungu mkono wako namna *hii*, kama hatufahamiani, pungu mkono wako huku na huku kama sikujui.

²²³ Mnaona? Hivi hamwamini? Mna shida gani ninyi Wapentekoste? Kwani hamjui Kristo ni nini? Mnataka kuponywa? Basi simameni kwa miguu yenu na muukubali. Na—nawapa changamoto muamini Jina la Yesu. Simameni, wekeaneni mikono, na mkubali uponyaji wenu. Kumbuka, ni wewe, wewe ndiwe. Unaamini kwa moyo wako wote?

Mwinulieni Kristo mikono yenu sasa na hebu tuombe. Wewe omba mwenyewe, jiombee wakati ninapowaombea.

²²⁴ Baba wa Mbinguni, ninakupa Wewe kusanyiko hili la watu katika Jina la Yesu Kristo, mponye kila mmoja wao, Bwana, jalia Roho Wako na nguvu zije juu yao na kuwaponya, kwa utukufu wa Mungu na kwa ajili ya utukufu wa Mungu ninaomba, katika Jina la Yesu Kristo.

²²⁵ Kila mwenye dhambi aliye hapa ndani usiyemjua Mungu kama Mwokozi wako, hivi hutakuja hapa juu na kumkubali Yeye kama Mwokozi wako sasa? Panda uje huku sasa, ninakupa changamoto uje huku sasa na umpokee Kristo kama Mwokozi wako. Utakuja? Usiyeamini, hiyo ilikuwa muda mfupi uliopita, na unataka kukubali?

Mungu awabariki, mabwana, njoni moja kwa moja. Jambo ndilo hilo kijana, ndivyo hivyo. Loo, hiyo ni kweli.

²²⁶ Ninyi ambao hamkuamini dakika chache zilizopita, na sasa mnataka kumwomba Mungu awasamehe kwa ajili ya kutokuamini kwenu, njoni kuizunguka madhabahu. Njoni sasa.

Amini tu, amini tu,

Mungu wabariki watu hawa wanaokuja.

Mambo yote yanawezekana, (. . . ? . . .)

Mambo yote yanawezekana, amini tu.

²²⁷ Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Lutheri, Katoliki, Wapentekoste, ambao hawaamini, njoni sasa madhabahuni, njoni tupate kuwawekea mikono wakati upako . . .

²²⁸ Ni kitu gani kingine kingeweza kufanya hivyo? Watu hao wote walioitwa kwenye mstari huo, popote pale, kama hatufahamiani, inueni mikono yenu, wale walioitwa mstarini, inueni mikono yenu. Hao hapo. Mnaona? Siwajui watu hao.

²²⁹ Roho Mtakatifu, mnajua alichoniambia? “Fanya wito wa madhabahuni sasa hivi. Kuna kutokuamini kwingi hapa ndani.” Hata nisingeweza kuuendeleza huu mkutano mpaka tuondoe kitu hicho hapa. Kuna shida gani? Ondoka! Hutaki roho kama hiyo karibu nawe. Vipi kama Yesu angeweza kuja Mwenyewe usiku wa leo, ninyi mnaoketi huko nje? Ninyi msioamini, njoni!

Mambo yote yanawezekana, amini tu.

Amini tu, amini tu,

Mambo yote yanawezekana . . .

²³⁰ Njoni. Njoni moja kwa moja sasa, kila mmoja wenu. Kama Kristo yuko karibu hivi nanyi katika Uwepo huo, kwa nini ubaki nyuma? Umekuwa na hisia ndogo ya kushuku, iondoe kwako, njoo sasa!

. . . amini tu,

Mambo yote yanawezekana, amini tu.

Amini tu . . .

Hivyo tu ndivyo anavyokuomba ufanye, kuamini, kuamini tu kwamba ni Yeye. Ninii tu, kama huamini jambo hilo, njoo huku ukatubu, angalia litakalotukia.

. . . yanawezekana, amini tu;

Amini tu . . .

Njoo, dada, ndivyo hivyo. “Yeye aendaye akitoa machozi bila sha- . . .atarudi akipiga kelele za furaha, akileta miganda ya thamani.”

Mambo yote yanawezekana, amini tu.

Nina furaha kuona wachungaji wakija, wakiwa tayari kukiri kwamba wamekosea.

Amini tu . . .

²³¹ Mungu ataheshimu maungamo safi yasiyoghoshiwa, bila shaka atayaheshimu. Utafanya nini wakati Roho yuyu huyu, hapa usiku wa leo, utasimama mbele Zake kuwajibika kwa ajili yake kwenye Siku ya Hukumu? Basi kumbukeni, liko kwenye wakati wake kabisa. Hivyo ndivyo alivyosema atafanya, nalo hili hapa.

. . . amini tu;

Mtakuja sasa, wengine zaidi?

Amini tu . . .

²³² Ninawapa uhuru, ninawapa uhuru kutoka kwa kutokuamini kwenu kwote, kama mtakuja kwa uaminifu, na kutubu, na kumkubali Kristo. Kama wewe ni mshirikina, mfuasi wa kanisa, hujui kama uko sahihi au la, afadhali uje.

. . . amini tu.

²³³ Sasa, wafanyakazi wa kibinafsi, njoni, wafanyakazi wote wa kibinafsi, mnaweza kuja moja kwa moja sasa, mpate kujua la kuwafanyia hawa watu, ninyi wafanyakazi wa kibinafsi, njoni moja kwa moja huku na kuwazunguka sasa, watu hawa hapa, kwa sababu tutakuwa na maombi.

²³⁴ Na kama kuna wasioamini huko nyuma nao wanataka kuja pia, wewe njoo moja kwa moja mbele kwa vyovyote vile. Kwa kusonga mbele usiku wa leo, enyi watu, umekiri kwamba una imani kwamba umekosea katika dhana yako, nawe unakuja sasa kupata tukio la Mungu aliye hai. Mungu yuyu huyu mnayemwona hapa akifanya kazi hapa jukwaani na kupitia kwa watu huko nje, Yeye ni Mungu wenu, wewe—wewe, labda wewe unaninii tu—hujasimama tu kwa dakika moja kulitafakari.

²³⁵ Yeye yupo hapa, Yeye Ndiye aliyekuita uje huku juu. Unaona? Roho yeye yule aliyenitia mafuta kuihubiri Injili Ndiye Yule yule aliyepitia kwenye kusanyiko kule, anayekujua, ungeweza kumgusa Yeye kwa mambo ya ninii, udhaifu wako.

²³⁶ Watu, bila shaka yoyote, watu ambao sijawahi kuwaona maishani mwangu, wanasimama huko nje, usiku baada ya usiku kupitia kwenye kusanyiko, wanakuja hapa jukwaani, usiku baada ya usiku, siku baada ya mwaka, juma baada ya juma, uamsho baada ya uamsho, na kamwe halishindwi hata wakati mmoja. Kama hiyo ni kweli, enyi kanisa, semeni, “Amina.” Basi, ni kwa nini Bwana . . .

²³⁷ Hebu niwaambie, BWANA ASEMA HIVI: Afadhali mtubu, Chicago. Saa yenu imekaribia. Tubuni! Njoni, mwamini, maana utakuja wakati ambapo utalilia hili, wala halitakuwepo. Hutapokea kilicho *halisi*, kwa hiyo kutakuwa na cha uongo utakachopewa. Yesu alisema, “Nimekuja katika Jina Langu Mwenyewe, hamnipokei, mwingine atakuja nanyi mtampokea.” Kumbukeni, ninanukuu Maneno Yake, yako kwenye kanda, kwenye kumbukumbu.

²³⁸ Afadhali umpokee wakati unapoweza, maana kuna mambo mengi ulimwenguni ambayo yako tayari kutimia. Wadudu ambao hawajawahi kuanguliwa hapo awali watatokea. Sasa ndio wakati wa kujiweka sawa, afadhali ufanye hivyo kabla . . . ndipo ninii, baada ya kitambo kidogo, kiti cha rehema kitaondolewa, wala hakutakuwako na ukombozi tena, kwa hiyo njoo uwezapo. Kama kuna chembe moja ya Mungu inayokuita, jitokeze sasa hivi.

Ili nipate kuwa na hakika, hebu niwe na hakika, mara nyingine tena, *Amini Tu*, sote pamoja.

Tu . . .

Ninaendelea kuhisi kuna mtu huko nje ambaye . . . mtu fulani mahali fulani.

. . . tu . . .

. . . mambo yanawezekana, tu . . .

²³⁹ Mimi si mlokole, jamani, kusema jambo fulani ambalo simaanishi kabisa moyoni mwangu. Hakika msingewazia hayo kulingana na yale Bwana aliyofanya. Hili hapa kundi zima la wasichana matineja linakuja.

Sasa, mambo yote yanawezekana, amini tu.

²⁴⁰ Sasa, ninawatakeni ninyi wafanyakazi wa kibinafsi, muwawekee mikono, kila mmoja wenu aweke, weka tu mikono yako juu ya mtu mwingine ili wewe, kama tu vile Ndugu yetu Oral Roberts amesema, mahali pa mawasiliano. (Hamna nafasi hapa ya kuwaweka, sivyo? La, sidhani wanayo.) Katika mikutano ya namna hii, wakati mwingine tunapokuwa nao, mwajua, tunatenga mahali ambapo tunaweza kuwa na vyumba kwa ajili ya ushirika.

²⁴¹ Nataka wasikilizaji wote mwinamishe kichwa chenu kila mahali, tafadhalini, ninyi huko nje mnaopenda nafsi hizi hapa madhabahuni, mkijua ya kwamba wamekuja kwa uchaji, usiku wa leo, kukiri makosa yao na—na kuomba msamaha, ili Mungu awarehemu. Bila shaka.

²⁴² Nakisia mnashangaa ni kwa nini ninaendelea kuweka mikono yangu juu ya *hivi* hapa. Mimi si mshirikina, mara kwa mara ninaangalia nje na kuona ono, na halafu wakati, naona watu huko nje wanaoamini na kuponywa, na hiyo ndiyo sababu ninaweka mikono yangu juu ya *hiki*, wakati huo. Mnaona?

²⁴³ Ndugu, dada, hivi unaweza kuvurugikiwa akili vya kutosha kuamini ya kwamba mtu angeweza kusimama hapa na kufanya jambo fulani, aende huko nje kwenye kusanyiko hilo, mwanadamu akiwa na . . . mwanadamu tu, na ati aende huko nje na kujua watu wanateseka na ni wagonjwa, na kadhalika? Ungeweza? Hilo—hilo haliwezekani. Ndio mwujiza mkubwa sana uliowahi kutukia katika miaka elfu mbili. Bila shaka.

²⁴⁴ Vema, ungeweza kufikiria juu ya ugonjwa wa akili, kama mtu alisimama kutoka kwenye kiti cha magurudumu na kuondoka, hilo—hilo limefanywa, hakika. Lakini niambie mahali nguvu, nionyeshe ambapo mtu fulani mwenye Ph.D., anaweza kuja hapa kwenye jukwaa hili, na kutembea huko nje kwa Roho Mtakatifu, na kuwaambia watu hao mambo hayo kama tu Roho Mtakatifu alivyofanya usiku wa leo, kama Yesu Kristo alivyofanya alipokuwa hapa. Niambieni mahali alipo,

mleteni hapa jukwaani kesho usiku, nitakuwa nikimtarajia. Mnaona, hayupo hapa; Huyo ni Roho Mtakatifu.

²⁴⁵ Na hao wagonjwa, hao Wakristo huko nje, ambao wanaomba, nao wanamgusa Yesu Kristo. Na kwa karama ya Kiungu Yeye yupo, ninaangalia tu kule na kuwaona, kuna Nuru juu yao, inaenea tu, nami ninaona wao ni nini na ni akina nani, mimi, kama tu ninavyowaangalia ninyi hapa, bali nawaona mahali pengine, wakifanya jambo fulani, ndipo basi ninazungumza tu, halafu ninapomaliza kuzungumza, sijui nimesema nini. Mnaona? Ni kama tu ndoto iliyoniondokea. Lakini hilo hapo, ni vile hasa Mungu alivyosema angefanya. Ninamwomba kasisi yeyote alikanushe, huwezi kulikanusha, kwa sababu liko papa hapa katika Biblia, BWANA ASEMA HIVI. Mnaona? Nalo hili hapa kwenye ile saa.

²⁴⁶ Sasa, mnasimama hapa, mkitubu, mnataka kuwa sawa na Mungu; ninataka kukutana nanyi katika Nchi bora kuliko hii ilivyo, siku moja. Nami na—nawaambia, ndugu yangu, dada, Kristo angali hai, Kristo yuko hapa. Tuko kwenye... karibu na mwisho wa wakati, kwangu mimi, ninaamini Yeye anakuja katika kizazi hiki, ninaamini kizazi hiki kitamwona Yesu akija, ninaamini kwa moyo wangu wote. Kwa namna fulani ninahisi ya kwamba huenda nikamwona akija, nami ni m—mzee, ningali ninaamini huenda nikamwona akija.

²⁴⁷ Sasa, ninataka kila mtu humu ndani uombe kwa njia yako mwenyewe, uungame makosa yako, useme, “Mungu, samahani.” Na kila mmoja humu jengoni, ninyi mlio na dhambi mliosimama hapa, msemi, “Mungu, nisamehe, ninataka kuwa Mkristo tangu usiku wa leo na kuendelea.”

²⁴⁸ Nanyi mlio hapa mnaokiri ya kwamba mmekuwa wavivu wala ha—hamjaweza kulielewa, msemi, “Sasa, Bwana, mimi huyu hapa nimesimama, nimeufungua moyo wangu, nimekuinulia Wewe mikono yangu, imani yangu inakutazama Wewe.” Na unapofanya hivyo, basi ninaamini Mungu atakujaza na Roho Mtakatifu na kukupa Kitu kilicho halisi.

²⁴⁹ Kama Roho Mtakatifu yuko hapa ndani, kama kweli ulikuwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu, ndugu, hauna budi kushuhudia jambo *hili*, kwa sababu ni Roho Mtakatifu. (Sasa, peleka hili huko juu, ndugu yangu.) [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²⁵⁰ Vema. Sasa, sote tunataka kuinamisha vichwa vyetu kwa uchaji sasa na tuwe, omba tu kimyakimya kwa nafsi yako kwa muda kidogo tu.

Imani yangu inakutazamia Wewe,
Ewe Mwana-Kondoo wa Kalvari,
Mwokozi wa Kiungu;
Sasa, nisikie ninapoomba,
Ondolea mbali dhambi zangu zote,
Ee nijalie tangu leo

Niwe Wako kabisa!

Huku nikitembea kwenye mzingile wa maisha
wenye giza,

Na huzuni zimenizunguka, (Zinakuja.)

Uwe Kiongozi wangu; (Nichukue sasa, Bwana,
uwe Kiongozi wangu.)

Loo, amuru giza ligeuke kuwa mchana,

Futilia mbali machozi ya huzuni,

Wala usiniache nipotee kamwe

Kutoka Kwako kwenda kando.

²⁵¹ Ee Baba Mungu, ibada ya Jumatano usiku inakaribia kwisha, kuna watu mia mbili au zaidi, nadhani, wamesimama karibu na madhabahu hii, wanatubu, wanahitaji neema, wimbo mzuri wa kale unachezwa, *Imani Yangu Inakutazamia Wewe*, wanatambua, Bwana, ya kwamba mwanadamu awezi kufanya mambo haya, ya kwamba ni Wewe.

²⁵² Na kama vile Mikaya alivyokuwa, usiku wa leo, katika somo letu, alijua ono lake lilikuwa ni la Mungu, kwa sababu lilikuwa ni kulingana na Neno la Mungu, vivyo hivyo ninajua, Bwana, usiku wa leo, vivyo hivyo tunajua ya kwamba ono hili ni la Mungu, kwa sababu ni kulingana na Neno Lake.


²⁵³ Na hapa umesimama Uzao wa Ibrahimu, Kanisa teule, likitoka, wakitaka kuwa tayari kuja kwa El Shaddai, kupata nguvu kutoka kwa Mungu, kwa ajili ya kubadilishwa mwili wapate kumpokea huyo Mwana wakati atakapokuja. Ninaomba ya kwamba utawajalia, Bwana, usiku wa leo, kila mmoja wao, uwape shauku ya moyo wao. Msamehe mwenye dhambi, ukamrudishe aliyerudi nyuma, Bwana, ondoa mashaka yote moyoni mwa mwaminio, ifanye hii kuwa saa kuu, Bwana.

²⁵⁴ Ninaamini Wewe upo hapa, ninajua Wewe upo hapa, na Roho Wa—Wako anatenda kazi. Tunahisi utamu wa Uwepo Wako. Tunakuona Wewe ukipitia kwenye kusanyiko, ukifanya yale tu uliyosema ungefanya.

²⁵⁵ Sasa, Baba, tunakushukuru kwa kufanya jambo hili. Tunaamini, nami ninamchukua kila mmoja wa watu hawa wanaosimama kwenye madhabahu hii, kama mtumishi Wako ninasimama kati yao na mauti, ninasimama kati yao na kutokuamini.

²⁵⁶ Nami ninajitupa njiani, katika Jina la Yesu Kristo, na kumwambia Shetani ambaye amewafunga: Huwezi kuwashikilia tena.” Ninampa changamoto kila ibilisi aliyepo: Waache watu hawa! Toka ndani yao! Huwezi kuwashikilia tena, dhambi zao zimesamehewa, kutokuamini kwao kumetoweka. Wao ni watoto wa Mungu tangu saa hii, na kuendelea. Huduma yao ni, katika maisha yao itakuwa kuu, nguvu za Mungu zitafuatana nao kila mahali waendapo. Watakuwa watoto wa

Mungu tangu saa hii, na kuendelea. Shetani, ninazungumza nawe! Waache! Katika Jina la Yesu, toka ndani yao!

²⁵⁷ Sasa, kila mmoja, ikiwa mnaamini, inueni mikono yenu na mumpe sifa, nanyi mnaweza . . . kutoka hapa huru, usiku wa leo, katika Jina la Bwana Yesu. 

61-0426 Nabii Mikaya
Stephen Mather High School
Chicago, Illinois Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org